Sudan Kusini

Kitabu cha mwanafunzi

# Kiswahili 3

**Kiswahili kwa kidato cha Tatu(3)** kimeandikwa na wizara ya Elimu na Mafunzo kwa jumla, Ikishirikiana na wataalam wa lugha.

Kitabu hiki kinamwelimisha mwanafunzi kwa mazoezi na vitendo.

**Kila darasa linajumuisha Kitabu cha Mwanafunzi na Mwongozo wa Mwalimu.**

**Kila Kitabu cha mwanafunzi kinakupa:**

- Ufafanuzi mwafaka wa mtaala wa kitaifa.
- Msingi bora katika kiswahili.
- Uwasilishaji na ufafanuzi wa hoja unazotakiwa kujifunza.
- Mazoezi mwafaka yanayoonyesha jinsi Kiswahili Kinaweza kutumika katika mifano halisi maishani.
- Fursa ya ushirikiano kupitia kwa kazi ya vikundi.
- Michoro ya kusisimua.

**Masomo yote katika mfululizo huu wa msingi yalitengenezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Mkuu, Jamhuri ya Sudan Kusini.**

**Vitabu vimeundwa kutekeleza somo la shule za msingi,na wakati huo huo kuwawezesha wanafunzi na ujuzi unaofaa katika jamii ya kisasa ya kimataifa**

**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kitabu kitakachopatikana kikiuzwa kwa njia yoyote kitatawaliwa na muuzaji kuchukuliwa hatua za kisheria.**

**Funded by:**

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION
quality education for all children

Kiswahili

Kidato Cha Tatu


Sudan Kusini

THE REPUBLIC OF SOUTH SUDAN
MINISTRY OF GENERAL EDUCATION AND INSTRUCTION

Kitabu cha mwanafunzi

# Kiswahili 3

Kidato cha Tatu



**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kimefadhiliwa na:**

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION
quality education for all children

# Jinsi ya kutunza kitabu chako.

**Mambo muhimu ya kuzingatia.**

1. Unaombwa kuhakikisha umenawa mikono kabla ya kukitumia kitabu chako.
2. Tumia kalamu ya rangi kuonyesha kazi iliyofanywa.Usikunje karatasi za vitabu.
3. Kitabu kikiharibika,hakikisha kinakarabatiwa kwa haraka.
4. Kuwa mwangalifu wakati unapomwazimu mwenzako kitabu.
5. Tafadhali kiweke kitabu chako mahali pakavu na pasipokuwa na unyevu.
6. Unapokipoteza kitabu chako, mjulishe mwalimu wako.

**Mambo unayokatazwa kufanya.**

1. Usiandike ndani au juu ya kitabu chako.
2. Usikate michoro iliyokitabuni.
3. Usirarue kurasa zozote kitabuni.
4. Usikiache kitabu kikiwa kimefunguliwa.
5. Usikiweke kitabu chako kwenye mkoba uliojazwa vitabu zaidi.
6. Usikitumie kitabu chako kujifunika wakati wa mvua.
7. Usikikalie kitabu chako.

KIDATO CHA

# Sudan Kusini 3

# Kiswahili

## *Kitabu cha Mwanafunzi*

©2018, THE REPUBLIC OF SOUTH SUDAN, MINISTRY OF GENERAL EDUCATION AND INSTRUCTION. All rights reserved. No part of this book may be reproduced by any means graphic, electronic, mechanical, photocopying, taping, storage and retrieval system without prior written permission of the Copyright Holder.Pictures, illustrations and links to third party websites are provided in good faith, for information and education purposes only.

Ilifadhiliwa na:

Kitabu hiki ni Mali ya Wizara
Kimetadhiliwa na ya Elimu na Mafunzo.

**KITABU HIKI HAKIRUHUSIWI KUUZWA.**

## FOREWORD

I am delighted to present to you this textbook, which is developed by the Ministry of General Education and Instruction based on the new South Sudan National Curriculum. The National Curriculum is a learner-centered curriculum that aims to meet the needs and aspirations of the new nation. In particular, it aims to develop (a) Good citizens; (b) successful lifelong learners; (c) creative, active and productive individuals; and (d) Environmentally responsible members of our society. This textbook, like many others, has been designed to contribute to achievement of these noble aims. It has been revised thoroughly by our Subject Panels, is deemed to be fit for the purpose and has been recommended to me for approval. Therefore, I hereby grant my approval. This textbook shall be used to facilitate learning for learners in all schools of the Republic of South Sudan, except international schools, with effect from 4th February, 2019.

I am deeply grateful to the staff of the Ministry of General Education and Instruction, especially Mr Michael Lopuke Lotyam Longolio, the Undersecretary of the Ministry, the staff of the Curriculum Development Centre, under the supervision of Mr Omot Okony Olok, the Director General for Quality Assurance and Standards, the Subject Panelists, the Curriculum Foundation (UK), under the able leadership of Dr Brian Male, for providing professional guidance throughout the process of the development of National Curriculum and school textbooks for the Republic of South Sudan since 2013. I wish to thank UNICEF South Sudan for managing the project funded by the Global Partnership in Education so well and funding the development of the National Curriculum and the new textbooks. I am equally grateful for the support provided by Mr Tony Calderbank, the former Country Director of the British Council, South Sudan; Sir Richard Arden, Senior Education Advisor of DfID, South Sudan. I thank Longhorn and Mountain Top publishers in Kenya for working closely with the Ministry, the Subject Panels, UNICEF and the Curriculum Foundation UK to write the new textbooks. Finally, I thank the former Ministers of Education, Hon. Joseph Ukel Abango and Hon. Dr John Gai Nyuot Yoh, for supporting me, in my previous role as the Undersecretary of the Ministry, to lead the Technical Committee to develop and complete the consultations on the new National Curriculum Framework by 29 November 2013.

The Ministry of General Education and Instruction, Republic of South Sudan, is most grateful to all these key stakeholders for their overwhelming support to the design and development of this historic South Sudan National Curriculum. This historic reform in South Sudan's education system is intended to benefit the people of South Sudan, especially the children and youth and the future generations. It shall enhance the quality of education in the country to promote peace, justice, liberty and prosperity for all. I urge all Teachers to put this textbook to good use.

May God bless South Sudan. May He help our Teachers to inspire, educate and transform the lives of all the children and youth of South Sudan.



Deng Deng Hoc Yai, (Hon.)
**Minister of General Education and Instruction, Republic of South Sudan**

# YALIYOMO

MASWALA YA KITAIFA....................................................1

KILIMO....................................................................18

MITINDO YA MAVAZIYA KIAFRIKA...........................48

HUDUMA ZA DHARURA.............................................69

TEKNOLOJIA ...........................................................82

AJIRA.....................................................................97

# SURA YA 1

# MASWALA YA KITAIFA

## Mada Ndogo ya 1: Kusikiliza na kuzungumza

Kuna mazingira mbalimbali tunapoishi; kwa mfano ofisi za kiserikali, jeshi na kadhalika.Kila mazingira yana lugha inayotumika. Matumizi haya ya lugha kulingana na mahali huitwa sajili ya lugha.Sajili ya lugha hutegemea mambo kadhaa, kama vile cheo, umri, uhusiano na kadhalika.

### Sajili ya ofisi za serikali

Lugha ya ofisi za serikali inapaswa kuwa:

- Nyepesi inayoeleweka kwa wepesi.
- Inayolenga kinachozungumziwa.
- Yenye heshima.
- Yenye msamiati teule wa mazingira yenyewe,mfano ikiwa ni ofisi ya waziri maneno kama mheshimiwa,naibu wa waziri,karani na kadhalika.
- Haina utani.
- Hurejelea majina ya heshima mf.waziri, mheshimiwa, mkuu wa Idara na kadhalika.

## Sajili ya kisheria

Hutumia lugha:

- Yenye msamiati wa kale.
- Yenye istalahi maalum.
- Sentensi ndefu sana.
- Urudiaji wa maneno.

## Sajili ya msikitini/kanisani

Hutumia lugha:

- Nyepesi kwa njia moja.
- Hurudiarudia maneno.
- Hurejelea Biblia/Korani.
- Ni ya kuhukumu.
- Ni ya kurai.

**Soma mazungumzo yafuatayo:**



| | |
|---|---|
| Mhusika 1: | *All rise*! Mnaweza keti. |
| Mhusika 2: | Mhusika wa 3, unashtakiwa kwamba mnamo tarehe 6, mwezi wa Juni ulivunja kibanda cha jirani na kuiba kuku.Unakubali mashtaka au la? |
| Mhusika 3: | Ninakataa mheshimiwa. |
| Mhusika 2: | Ikiwa unakataa, eleza walio hapa kilichotokea siku hiyo. |
| Mhusika 3: | Mheshimiwa nina uchungu mwingi sana maana unavyoniona mimi sina mke…. |
| Mhusika 2: | Sikukuuliza kuhusu maisha yako, nimekwambia ueleze ya siku hiyo. |
| Mhusika 3: | Asante sana Mheshimiwa.Maisha yangu yamekuwa ya dhiki.Mnamo siku hiyo, nilikuwa nimeenda kumtembelea *friend* yangu. |
| Mhusika 2: | Nani *friend* yako? |
| Mhusika 3: | *Friend* yangu ni huyo anasema nilimwibia kuku.Sasa nilipofika kwake tulikaa, tukakaa, tukakaa, tuka… |
| Mhusika 2: | Eh! Wacha kuharibu wakati.Endelea na maelezo! |
| Mhusika 3: | Haya sawa Mheshimiwa, nilikuwa nataka kukuonyesha vile tulikaa, tukakaa, tukakaa…ndio, eh tukakaa, namaanisha kutoka saa tatu mpaka saa saba. |
| Mhusika 2: | Ndio, endelea. |
| Mhusika 3: | Saaasa huyu friend yangu sikuona akinipa chakula na vile nilikuwa nahisi njaa. |
| Mhusika 2: | Halafu kukatokeana nini? |
| Mhusika 3: | Saaasa friend yangu akatoka peke yake.Nilimchungulia darishani na nikamuona akikata mkate aliokuwa ameficha kwenye mfuko wa suruali yake. |
| Mhusika 2: | Kwa hivyo ukafanya nini? |
| Mhusika 3: | Mimi sikufanya kitu, nilingoja akarudi nami nikamwambia ninataka kuondoka.Tuliagana nami nikatoka. |
| Mhusika 2: | Endelea. Ulipotoka kulifanyikaje? |
| Mhusika 3: | Hakukufanyika chochote bali nilimwona kuku akichakurachakura hapo nje. |
| Mhusika 2: | Kuku wa nani? Endelea |
| Mhusika 3: | Sijui lakini nilimwongelesha akaninyamazia. |

| | |
|---|---|
| Mhusika 2: | Ukamwongelesha nani? |
| Mhusika 3: | Kuku! Nilimwambia ‘wewe, bosi yako amekataa kunimegea mkate, utanitambua. |
| Mhusika 2: | Wewe uko na akili timamu? Uliongea na kuku? |
| Mhusika 3: | Ndio mheshimiwa.Baadaye nikamkimbiza…huyo nami…huyo na mimi.Mwishowe nikamuweka mikononi, na nikaondoka naye.Sasa huko ndiko kuiba? |
| Mhusika 2: | Kulingana na maelezo yako uliiba kuku wa mwenzako, amepatikana na hatia na utafungwa miaka miwili na kazi ngumu iwe funzo kwa wengine. |
| Mhusika 3: | Lakini si kuiba, nilichukua… |
| Mhusika 2: | Nyamaza.Askari? Tupa huyu ndani. |
| Mhusika 1: | *Simameni nyote*. |

## ZOEZI

1. Tambua sajili hii.
2. Tambua mhusika wa 2 na wa 3.
3. Taja sifa kumi za sajili hii.
4. Taja msamiati teule wa sajili hii uliotumika katika mazungumzo haya.
5. Kulingana  na mazungumzo haya wahusika hawa wanaitwaje kulingana na sajili hii:mfano mhusika 1 ni Askari
   a) mhusika wa 2.
   b) Mhusika wa 3.
   c) Yule anarejelewa kama ‘’my friend’’

**B)** Beba! Beba! Wale wanataka uhondo waingie! Beba! Beba! Dereva kanyanga breki! Twende mama, twende mrembo,
Beba! Beba! Wachwa huchekwe!!

## ZOEZI

1. Tambua sajili hii.
2. Sajili hii huwana porojo nyingi.Thibitisha kwa kutaja maneno kadhaa kwenye kifungu.

3. Taja sifa tano za sajili hii.
4. Taja msamiati teule **tano**wa sajili hii.
5. Andika kisa cha mazungumzo baina ya watu wawili juu ya matumzi ya sajili hii.

## C) Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.

Y: Hujambo!
Z: Sijambo.Ninaweza kuingia?
Y: Ndio, ingia.Jana sikukuona.Ulikuwa wapi?
Z: Asante.jana nilikuwa mgonjwa na mamangu akanipeleka hospitali.
Y: Pole.Wapi kadi ya kutibiwa?
Z: Ndiyo hii, shika tafadhali.
Y: Sawa nimeisoma na kuthibitisha ni kweli ulienda hospitali.Wakati hukuwepo niliwapa wenzako zoezi la Sarufi.Fanya na uniletee nisahihishe saa hii.
Z: Ndio, nitafanya hivyo, tafadhali

## ZOEZI

1. Tambua mhusika Y na Z.
2. Je hawa wahusika wako wapi? Thibitisha.
3. Dondoa maneno kutoka kwa kifungu yanayoonyesha heshima.
4. Kulingana na kifungu taja sifa za mhusika Z.
5. Taja sifa **saba** za sajili hii.

D) Orodhesha sifa kumi za:

a) sajili yamagazeti.
b) sajili ya hospitali.

**Mada Ndogo ya 2:** **Kusoma**

## SAJILI YA DINI

Jamii mbalimbali hutumia lugha kwa njia tofautitofauti kuelezea dini.Lugha ya dini huwasilishwa kupitia kwa maandiko yanayoaminika kuwa matakatifu.Maandiko haya ni kama ya kuran na biblia.Pia kupitia kwa nyimbo za injili na mahubiri, lugha ya dini huwasilishwa.

Lugha ya dini yoyote ile huwa na sifa kama vile matumizi ya msamiati wa kikale.Ijapokuwa siku hizi maandishi ya kisasa yanatumika katika maandiko ya maswala ya kidini, bado lugha ya kikale inatumika katika dini zote.Matumizi haya ya kikale yanasaidia kuhifadhi ujumbe maalum uliokuwepo tangu jadi. Hii inarithisha vizazi vyote viweze kuupata ujumbe wa dini yao kwa njia mahususi.

Dini zote huteua lugha sahili inayoeleweka na waumini wake ili waweze kupata ujmbe uliokusudiwa.Dini hazitumii maneno au dhana za kitaalamu ambazo hazieleweki na waumini wake.Huenda msomaji akajiuliza,je, Waislamu wanaotumia Kiarabu kwa dini yao,wanakielewa?Jibu nindio.Wanaelewa kabisa na mahubiri na maombi katika lugha ya Kiarabu.Wanaweza kutafsiri wanachokisema kwa kiarabu bila kupotosha waumini wao.

Msamiati wa lugha ya kidini huwa maalum.Majina yanayotofautina humaanisha kitu kimoja; Mfano Koranikwa Waislamu na Biblia kwa Wakristo yaani kitabu kitakatifu.Mola ndiye Mungu, Yahweh Mwenyezi.Msamiati mwingine niunakuwa sawa kama vile dhambi, utakatifu na kadhalika.

Lugha ya kidini huegemea kwa dhana ya Mungu.Katika mahubiri, maombina shughuli za kidini ni lazima dhana ya Uungu ijitokeze.Dini zote zinachukulia Mungu kama mwenye uwezo wote na hivyo hutambulikana kwa vyovyote vile.

Sajili ya dini hutumia lugha ya kuonya na yenye ukali.Ijapokuwa katika dini kuna dhana naimani ya msamaha,maneno katika sajili hii huonya na kuhukumu;kwa mfano,Korani/Biblia inasema sema anayetenda dhambi atahukumiwa.Hutumia lugha bila kuficha ukweli wa mambo mfano mshahara wa dhambi ni mauti!

Hata hivyo, kwa upande mwingine,sajili ya dini huwa ya kuliwaza.Ni sajili yenye msamaha na matumaini.Inasema ukitubu dhambi zako utasamehewa.Ina maneno na majina ya upendo kama; ndugu, dada, wapendwa.

Matumizi ya lugha ya adabu, upolena kutasfidi hutumika.Maneno yaliyo ya aibu hupewa maana fiche; mfano kitendo cha kimapenzi huitwa kujuana kimwili.Ni lugha ya kunyenyekea na upole kama vile "ndugu zangu tubuni dhambi msihukumiwe''.

Mwisho sajili ya dini imejaa ushauri mwingi.Inaelekeza na kushauri mtu juu ya mambo yote ya maisha.Ina ushauri wa ndoa, familia, marafiki, ufanisi, maafa na kadhalika. Husimulia mambo haya yote kwa njia tofautitofauti kama kisa, mafumbo, masimulizi au maelezo ya moja kwa moja.

**MASWALI**

1. Taja mifano minne ya maandishi ya dini.
2. Lugha ya dini imebadilika vipi?
3. Taja umuhimu wakutumia lugha ya kale katika dini.
4. Toa thibitisho ya kueleweka kwa matumizi ya Kiarabu na Waislamu katika dini yao.
5. Mwandishi anposema ''msamiati wa lugha ya kidini huwa maalum''anamaanisha nini?
6. Taja sifa za Mungu kulingana na kifungu.
7. Kulingana na dini yako, thibisha hoja kuwa sajili ya dini hutumia lugha yenye ukali.
8. Undugu unajitokezaje kwenye sajili ya dini?
9. Taja maneno ya kutasfidi unayoyajua katika sajili ya dini yako.
10. Kando na yaliyotajwa kwenye kifungu orodhesha sifa za sajili ya dini.

## Mada Ndogo ya 3: Sarufi

### VITENZI

Haya ni maneno yanayosimamia kitendo. Kila kitenzi huwa na shina la kitenzi (sehemu ndogo Zaidi ya kitenzi ambayo huwakilisha tendo hilo). Shina la kitenzi huambatanishwa na viambishi ili kutoa maana iliyokusudiwa kama vile mtendaji, mtendewa, wakati wa kitendo kufanyika na pia kauli ya kitenzi hicho.

#### Aina za vitenzi

1. Vitenzi halisi
2. Vitenzi vikuu
3. Vitenzi visaidizi
4. Vitenzi vishirikishi
5. Vitenzi sambamba

#### Vitenzi halisi

Hivi ni vitenzi vinavyorejelea kitendo moja kwa moja. Vitenzi hivi huarifu mambo yafuatayo:

1. Tendo linatendeka. Mifano: soma, cheza, lia, cheka, lima n.k.
2. Wakati wa kutenda jambo. Mifano: wanasoma, walisoma, watasoma.
3. Hali ya kitenzi.
4. Kauli ya kitenzi
5. Uyakinishi au ukanushi

## Vitenzi vikuu

Kitenzi kikuu ni aina ya kitenzi halisi. Kitenzi hiki hueleza tendo lililofanywa na tendo au alilofanyiwa mtendwa, wakati wa tendo lenyewe, hali ya tendona kauli ya tendo hilo.

## Vitenzi Visaidizi

Vitenzi visaidizi hutangulia vitenzi vikuu katika sentensi ili kuleta maana inayokusudiwa kulingana na wakati au hali.

**Mifano:**

1. Mama alikuwa amechoka sana.
2. Mtoto angali analala.

## Vitenzi vishirikishi

Hivi hutumika kuelezea hali iliyopo au mazingira.

Mifano:

1. Mkulima yu shambani.
2. Mwalimu si mjinga.

## Kuna aina mbili za vitenzi vishirikishi.

a) Vitenzi vishirikishi vikamilifu

Vitenzi hivi huchukua viwakilishi nafsi au viambishi ngeli na vilevile viambishi vya wakati. Mifano:

1. Walimu walikuwa wangali mkutanoni.
2. Mchezaji amekuwa stadi.

b) Vitenzi vishirikishi vipungufu

Vitenzi vya aina hii havichukui viambishi vya wakati ingawa ninaweza kuchukua viwakilishi nafsi au viambishi ngeli. Vitenzi hivi ni si, ni, ndi- na viwakilishi nafsi visimamapo peke yake. Mifano:

1. Yeye ndiye mwalimu mkuu katika shule hii.
2. Wao si watu wakakamavu.

3. Wewe ni mwanfunzi mtukutu sana.

### Vitenzi sambamba

Vitenzi hivi hutokea katika mfululizo. Mfululizo wa aina hii unaweza kuleta pamoja kitenzi kisaidizi au kishirikishi na kitenzi halisi; huweza pia kuhusisha vitenzi visaidizi kadha na kitenzi kikuu. Mifano:

1. Deng *angali anasoma*.
2. Nyinyi *mtakuja kujuta*.
3. Kame *alikuwa akienda shuleni*.

### Zoezi

1. Tofautisha kati ya vitenzi visaidizi na vitenzi vikuu.
2. Tunga mifano mitano kuonyesha:
   **a)** Vitenzi vishirikishi
   **b)** Vitenzi halisi

## Mada Ndogo ya 4: Ufahamu

## Ushairi

Shairi ni mtungo wa kisanaa. Utungo huu hufuata kanuni fulani za utunzi.

### Vipengele muhimu katika utunzi

Shairi huundwa kwa silabi ziitwazo mizani. Mizani huunda neno au maneno ambayo yakifululizwa huunda sentensi zinazoitwa mshororo (umoja) au mishororo (wingi).

Ukamilifu wa mishororo kadhaa huunda ubeti (umoja) au beti (wingi). Mshororo wa ubeti unaweza kugawika katika vipande kadhaa au unaweza kufululizwa

ikiwa mshororo umegawika katika sehemu tatu, kipande cha kwanza huitwa ukwapi, cha pili utao na cha tatu mwandamizi.

Silabi za kila nusu mshororo au za mwishoni mwa kila mshororo huitwa vina. Vina vinaweza kuwa vya kati (ndani) au vya nje (mwisho).

**Mfano:**

Wewe kiumbe malaika, kakuumba nani?
Macho yangu ya'angaika, kakuumba nani?
Mtihani mi 'taanguka, kakuumba nani?
Kweli jawabu hakuna.

Ubeti huu una mishororo minne.
Mishororo ya ubeti huu imegawika kuwili; ukwapi na utao.
Mizani upande wa ukwapi ni 8 na upande wa utao ni 6. Mshororo wa mwisho una mizani 8 pekee. Vina katika ukwapi ni ka, na vya utao ni ni. Kina cha kibwagizo ni na.

## Aina za Mashairi

Baadhi ya vipengele vya kuzingatia ili kueleza mkondo wa shairi ni urefu wa mada ya shairi, mishororo katika kila ubeti na ikiwa shairi ni la majibizano. Kwa mfano:

a) **Tathmina:** Shairi lenye mshororo mmoja tu katika kila ubeti.
Tazama mfano:

Ubeti 1 _____________.

Ubeti 2 _____________.

b) **Tathnia**: Shairi lenye mishororo miwili katika kila ubeti. Tazama mfano:

Ubeti 1 _______________.
_______________.

Ubeti 2 _______________.
_______________.

c) **Tathlitha**: Shairi lenye mishororo mitatu katika kila ubeti. Tazama mfano:

Ubeti 1 _______________.

______________.

______________.

Ubeti 2 ______________.

d) **Tarbia**: Shairi lenye mishororo minne katika kila ubeti. Tazama mfano:

Ubeti 1 ______________.

______________.

______________.

______________.

Ubeti 2 ______________.

______________.

______________.

______________.

e) **Takhmisa:** Shairi lenye mishororo mitano katika kila ubeti. Tazama mfano:

Ubeti 1 ______________.

______________.

______________.

______________.

______________.

Ubeti 2 ______________.

______________.

______________.

______________.

______________.

f) **Tathlitha:** Shairi lenye mishororo sita katika kila ubeti. Tazama mfano:

Ubeti 1 ______________.

______________.

______________.

______________.

______________.

______________.

Ubeti 2 ______________.

______________.

______________.

_______________.
_______________.
_______________.

g) **Usaba:** Shairi lenye mishororo saba katika kila ubeti. Tazama mfano:

Ubeti 1 _______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.

Ubeti 2 _______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.

h**) Tasdisa:** Shairi lenye mishororo tisa katika kila ubeti. **Tazama mfano:**

Ubeti 1 _______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.

Ubeti 2 _______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.

_______________.
_______________.
_______________.
_______________.

**h) Ukumi**: Shairi lenye mishororo kumi katika kila ubeti. Tazama mfano:

Ubeti 1 _______________.
_______________.
_______________.
_____ _________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.

Ubeti 2 _______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.
_______________.

## Ngonjera au malumbano

Ni shairi lenye wahusika zaidi ya mmoja. Wahusika hawa hujibizana kuhusu jambo fulani. Mfano wa ngonjera:

Mwana: Kwako baba nauliza,
Wewe uliye nizaa,
Elimu muhimu gani?
Baba: Ewe mwana takujibu,

Kosa elimu mwana.
Takuja kulangu taabu,

**Utenzi**

Ni shairi refu sana linaloelezea kisa au historia ya mtu, mahali ama kitu fulani. Aghalabu kila mshororo katika utenzi huwa na urefu wa mizani chache kama vile nane.

Mfano; Ubeti 1 ___________8a
___________8a
___________8a
___________8b

Ubeti 2 ___________8a
___________8a
___________8a
___________8b

**Mishororo**

- Ubeti huundwa kwa mishororo au mshororo.
- Kila mshororo una jina lake.

1. Mwanzo: Mshororo wa kwanza katika kila ubeti.
2. Mloto: Mshororo wa pili katika kila ubeti.
3. Mleo: Mshororo wa tatu katika kila ubeti.
4. Kituo: Mshororo wa mwisho katika ubeti. Mshororo huu wa mwisho ikiwa unarudiwarudiwa katika kila ubeti, huitwa kipokeo, kiitikio, mkarara au kibwagizo. Ikiwa mshororo huu wa mwisho haurudiwirudiwi katika kila ubeti basi huitwa kimalizio au kiishio.

Mfano:

Ubeti 1 ___________ Mwanzo
___________ Mloto
___________ Mleo
___________ Kibwagizo

2 ___________ Mwanzo

___________ Mloto
___________ Mleo
___________ Kibwagizo

## Zoezi

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

**WASIA WA BABA**

1. Soma nakusihi kijana soma,
Vishindo maishani takusuma,
Kikosa elimu utalalama,
Kwa nini mwana husomi?
2. Mabuku tele 'fukoni kajaza,
Elimu najivunia kameza,
Ukikosa ujuzi tachokeza,
Kwa nini mwana husomi?

3. Mziki usiku haukuchoshi,
Kelele na vitushi hauishi,
Ba' ku'dhika hakukubabaishi,
Kwa nini mwana husomi?

4. Onyo mwanangu nakupa mapema,
Jikaze vitabuni na kupema,
Hutakosa mwana kwa kweli mema,
Kwa nini mwana husomi?

**MASWALI**

1 (a) Chambua shairi ukizingatia:
**i)** Vina katika shairi hili.
ii) Mishororo ya kila ubeti.
iii) Mizani katika kila mshororo.
(b) Shairi hili ni la aina gani? Kwa nini?

(c) Ujumbe upi unaojitokeza katika ubeti wa kwanza na wa nne?

2. i) Shairi ni nini?
ii) Taja majina ya mshororo wa kwanza hadi wa mwisho.
iii) Kwa kuchunguza mishororo, mashairi ya mishoro ifuatayo huitwaje?

(a) _______________,
_______________,
_______________.

(b) _______________.

(c) _______________,
_______________,
_______________,
_______________.

(d) _______________,
_______________,
_______________,
_______________,
_______________,
_______________.

# SURA YA 2

# KILIMO

## Mada Ndogo ya 1: Kusikiliza na kuzungumza

### Kilimo Mufti

Mbele hapa ninaamba, maneno yenye busara,
Mambo yaende sambamba, ujikaze kila mara,
Kila siku utaimba, umepuka masihara,
Kilimo mufti nasema, ndio uti wa mgongo.

Malenga ninadokeza, kilimo msaidizi,
Bilashaka utaweza, kufaulu zama hizi,
Wakati hutapoteza, utavumbua ujuzi,
Kilimo mufti nasema, ndio uti wa mgongo,

Ninayo hoja ya mwaka, wewe tilia juhudi,
Mbolea utayaweka, seni kuwa na kusudi,
Utaepuka mashaka, mwenzangu ujifaidi,
Kilimo mufti nasema, ndio uti wa mgongo,

Japo yapo matatizo, swahibu ujizatiti,
Uzifuate vigezo, usitegeme bahati,
Hakika una uwezo , vipengele madhubuti,
Kilimo mufti nasema, ndio uti wa mgongo,

Nchi yangu naienzi , kilimo kaiboresha,
Ama kweli hizi enzi , mkulima  kafanikiwa,
ukulima ulio stadi,Kwa yakini ni kurunzi,
Kilimo mufti nasema, ndio uti wa mgongo.

Tafuta walobobea, wanofahamu tijara,
Bahari waogelea, wameshakuwa imara,
mkulima kavumilia, apata kwayo ajira,
Kilimo mufti nasema, ndio uti wa mgongo.

Ninakunja jamvi langu, nimeboronga ya kweli,
Utoe dua kwa Mungu, nachamba miye mswahili,
Farisi wa ulimwengu, yaache mengi maswali,
Kilimo mufti nasema, ndio uti wa mgongo.

## MASWALI

1. Mwandishi anajivunie nini katika shairi nzima?
2. Mshairi antuhimiza tutumie nini katika ubeti wa 3?
3. Ubeti wa 4 unaongea juu ya nini?
4. Nini kinaitwa kurunzi katika ubeti wa 5?
5. Andika maana ya maneno yafuatayo:
    a) Masihara
    b) Mufti
    c) Vigezo
    d) Dua
    e) Ajira

## ACHANIKAYE JUANI

Asubuhi kumekucha, amka sijikunyate,
Siwaze kiuma kucha, hutoshibishwa na mate,
Jichemshie mchicha, utolezee mikate,
Achanikaye juani, hujilia uvulini.

Hangaika usichoke, ukaja ukakufuru,
Kufuru zisikutoke, upatacho ushukuru,
Shukuru usipotoke, maovu yakakudhuru,
Achanikaye juani, hujilia uvulini.

Dada ndani usirembe, jikaze kikakamaa,
'Nimechoka' usiambe, katafute vidagaa,
Ukirudi ule sembe, usije ukafa njaa,
Achanikaye juani, hujilia uvulini.

Binadamu kujituma, ni faradhi ya uhai,
Ukipanda utachuma, mavuno yakukinai,
Mwindaji akifuma, kitoweo hakikai,
Achanikaye juani, hujilia uvulini.

Mkulima mwenye jembe, hodari ulokomaa,
Kalime usiwe zembe, shambani hapatazaa,
Uvune japo maembe, na mboga zilozagaa,
Achanikaye juani, hujilia uvulini.

Atafutae riziki, hachoki akapumua,
Sipopata hadiriki, akakaa na kutua,
Kila mja ana dhiki, juhudizo zitafua,
Achanikaye juani, hujilia uvulini.
*Limenukuliwa kutoka mashairi ya HAMZA A.MOHAMMED*

## MASWALI

1. Eleza maudhui ya shairi hili.
2. Ni nini mshairi anawaonya wasichana katika ubeti wa 3?
3. Andika ubeti wa 5 kwa lugha ya kawaida.
4. Nini maana ya ‘’kipanda utachuma’’?
5. Mwandishi anamlenga nani katika shairi hili?

## Mada Ndogo ya 2: Kusoma

**Kifungu A**

### KILIMO

Kilimo ni kazi ya kulima na kupanda mimea shambani.Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa wataifa lolote lile.Wakulima hufanya shuguli zao za upanzi kulingana na misimu.Wao huyatarisha mashamba yao wakati wa kiangazi.

Matayarisho hayo huwani; kufyeka, kungoa visiki, kulima na kadhalika.Msimu huo wao hupanda. Mbali naupanzi na ukuzaji wa mimea, baadhi ya wakulima pia hujishughulisha na ufugaji wa mifugo. Mifugo hao ni kama vile ngombe, kondoo, mbuzi, nguruwe na sungura.Hali kadhalika, wao hufuga ndege kama kuku na bata. Mifugo huwa na faida kochokocho kwa mwanadamu mathlani mayai na nyama kutoka kwa ndege, maziwa, ngozi namafuta kutoka kwa mifugo.

Mimea mbalimbali hukuzwa kwa ajili ya chakula. Hii ni mimea kama vile mhindi, maharagwe, miembe na kadhalika. Licha ya hayo, kuna mimea ambayo hukuzwa kwa ajili ya kuuzwa kama vile pareto, kahawa, chai na pamba. Mimea kama vile pareto pia hutumiwa nchini kutengenezea dawa za kunyinyuzia

wadudu waharibifu. Mpamba pia hutumiwa katika viwanda vya kutengeza nguo, ingawa zao hilo limedidimia nchini.

Licha ya kujishughulisha na kilimo cha chakula, watu pia huendeleza kilimo cha ufugaji. Baadhi ya jamii, hasa zile zinazohamahama hufuga mifugo wengi kama vile ng’ombe. Wengine hufuga ng’ombe wachache kwa minajili ya kupata maziwa ya matumizi yao ya kila siku na ya kuuza ili kupata pesa za kukidhia mahitaji mengine. Aidha, kuna wale ambao hufuga ng’ombe, mbuzi, kondoo na hata nguruwe kwa ajili ya nyama.

## Wanyama wanaofugwa



Mbwa




Paka



Nguruwe



Mbuzi





Ng’ombe

Kondoo



Kuku





Punda

Farasi

Wengine pia hufuga kuku kwa ajili ya mayai na nyama. Kutokana na shughuli hizi, watu wameweza kupata pesa za kutosheleza mahitaji yao naya familia zao.

Isitoshe, watu wengine wamekuwa wakijishughulisha na kilimo cha bustani. Wamekuwa wanapanda maua na mboga kwa ajili ya matumizi nchini na kwa kuuza ng'ambo. Kwa njia hii, wananchi hawa wameweza kuiinua nchi kiuchumi.

Kilimo ni sekta muhimu mno katika uchumi wa chi yetu. Nchi isiyoweza kujilisha ni nchi dhaifu isiyoweza kutegemewa. Ni muhimu kustawisha kilimo ili tuweze kupata chakula cha kulishia watu wetu, la sivyo tutabakia kuwa watu wa kuombaomba kila wakati bila kujua kuwa uso una haya.

Sekta ya kilimo pia huweza kutoa ajira kwa wananchi wengi iwapo itastawishwa. Ni dhahiri kuwa nafasi za kazi nchini zimekuwa haba kwa sababu ya ongezeko la idadi ya watu na pia ukuaji wa kikonokono wa uchumi wetu. Vijana wengi wanaohitimu masomo wamejikuta wakisombwa na mawimbi ya ukosefu wa kazi na hutupwa jijini ambamo hawaambulii lolote.

Tukistawisha kilimo katika sehemu za mashamabani tutaweza kupunguza kasi ya uhamiaji mijini ya watu na kukabiliana na msongamano wa watu mijini.

Sekta ya kilimo imekabiliwa na matatizo mengi ambayo yanatishia kuidumaza kabisa. Hali ya anga ambayo kamwe imekosa kutabirika imesababababisha hasara kubwa kwa wakulima. Majira ya kiangazi yamekuwa marefu na makali zaidi kiasi cha kusababisha kusalimu amri kwa mimea na mifugo.

Katika baadhi ya sehemu zingine si ajabu kupata mvua haijanyesha kwa misimu minne mtawalia. Hali ikiwa hivi mifugo hukondeana na kuwa vifefe, chakula nacho huadimika kabisa. Wananchi wa sehemu hizi wakabaki kunyongonyea na kutegemea ruzuku za chakula kutoka kwa jamii jirani na hata mataifa mengine.

Uhaba wa ardhi mwafaka ya kulima pia umechangia pakubwa kudidimiza kilimo. Wananchi wengi ambao wangependa kushika mpini hujipata wakilima visehemu vidogovidogo mno vya ardhi ambavyo haviwezi kumudu mahitaji yao.

Aidha, wengine wamekabiliwa na uhaba wa vifaa vya kisasa kama vile tingatinga na vingine vingi. Baadhi yao hawana pesa za kutosha kununulia mbolea na kuneemesha mazao yao. Kuna wale ambao hawatunzi ardhi zao vilivyo, wao hupanda kwenye miteremko na hawachimbi mitaro ya kuzuia mmomonyoko wa udongo. Mambo haya yote huyafanya mazao kuwa haba na wakulima wengi huwa hawana hamu ya kuendeleza kilimo.

Ukosefu wa njia bora za usafirishaji pia huwakatisha tamaa wakulima. Wale ambao huuza mazao kama vile mboga na mengine mengi kutoka sehemu za mashambani hupata kuwa mazao yao huweza kuharibika kutokana na ukosefu wa vyombo vya kusafirisha na gharama za juu za usafirishaji. Aidha wale wakulima wadogowadogo, hasa wanaofuga ng'ombe wa maziwa, hupata ushindani mkubwa kutoka kwa mapapa ambao tayari wamejikita.

Kwa njia hii wakulima hawa hukata tamaa na baadhi yao kulazimika kuuza mifugo. Wengine pia hukabiliwa na magonjwa ambayo huua mifugo kama na wale ambao hupanda mimea hupata hasara ya mimea yao kuvamiwa.Wale ambao hunuia kuuza maua yao ng'ambo hukwazwa na tatizo la fedha za kulipia ushuru. Kwa sababu ya tatizo hili, wao huazimia kuwauzia walanguzi maua yao ili waweze kuuza ng'ambo. Walanguzi hawa huwapunja wakulima hawa kwa kununua maua yao kwa bei duni ajabu. Kumekuwa na visa vya walanguzi hawa kutowalipa wakulima pesa zao. Jambo hili huendelea kuwadidimiza wakulima.

Ni wajibu wa kila mwananchi kuhakikisha kuwa kilimo kimepewa hadhi inavyostahili. Vijana ambao wanakebehi kilimo hawana budi kukumbushwa kuwa ndicho uti wa mgongo wanchi. Maafisa wa kilimo nao wawatembelee wakulima nyanjani mara kwa mara ili kuwaelekeza. Magonjwa ya mifugo na mimea yatafutiwe dawa na barabara za mashambani ziimarishwe. Ikiwa mambo hayo yote yatatekelezwa, tutaweza kuokoa fedha nyingi ambazo zinatumiwa kuagizia chakula kutoka nje na kuweza kustawisha sekta nyingine ili kuimarisha uchumi.

## MASWALI

1. Eleza maana ya “kilimo”.
2. Kulingana na kifungu upanzi hutegemea nini?
3. Mashamba hutayarishwa wakati upi?
4. Taja matayarisho matatu ya shamba.
5. Taja aina ya mifugo ambayo mkulima anaweza kufuga.
6. Kulingana nakifungu mimea imegawika kwa manufaa mawili.Yataje.
7. Taja mifano mitatu ya mimea ianayokuzwa kwaajili ya kuuzwa.
8. Eleza matumizi ya mmea:
    a) wa pareto.
    b) Pamba
9. Kilimo kimegawika mara mbili; zitaje.
10. Toa sababu mbili za kufuga mifugo wachache.
11. Nyama hupatikanakutoka kwa wanyama wepi?
12. Eleza maana ya kilimo cha bustani kulingana na kifungu.
13. Taja umuhimu wa kilimo cha bustani kwa nchi.
14. Eleza madhara ya kutozingatia kilimo kwa nchi.
15. Uhaba wa kazi umesababishwa na nini kulingana na kifungu?
16. Taja suluhisho mbili zitakazopatikana kutokana na kupata kazi mashambani.
17. Ni matatizo yepi yanayowakumba vijana waliohitimu masomo?
18. Taja madhara ya ukosefu wa ardhi ya kulima
19. Kulingana na kifungu majira ya kiangazi yanaathiri kilimo kwa nini?
20. Taja madhara mawili yanaoletwa na ukosefu wa mvua.
21. Taja vile wakulima wengine hawazingatii ukulima bora.
22. Kuna baadhi ya wakulima ambao wangetaka kulima lakini wanapata matatizo kadhaa.Yataje matatizo hayo
23. Wakulima wa mboga wanakabiliwa na changamoto zipi?
24. Wakulima wadogo wa kufuga ng’ombe hawapati soko kamili.Thibitisha.
25. Wauzaji maua wanapata shida mbili lipi la kifedha?
26. Walanguzi wa maua husababishia mkulima hasara.Eleza kulingana na kifungu.
27. Mwandishi ametoa himizo za kufanikisha kilimo katika aya ya mwisho. Zitaje.

**Kifungu B**

Jamhuri ya Sudan Kusini imefungua milango wazi kwa ajili ya biashara na nchi zingine.Baada ya zaidi ya miaka 20 ya kupigana vita, nchi mpya zaidi ulimwenguni ambayo ni Sudan Kusini iko tayari kwa uwekezaji na biashara.

Taifa la Sudan Kusini lina historia pana juu ya kilimo.Mnamo mwaka wa 1991 Sudan ilikuwa na sekta kubwa ya kilimo ya kunyunyizia mazao maji.Asilimia kubwa ya eneo la unyunyuziaji huu lilikuwa katika miradi ya serikali; kulikuwa na njia tatu za kunyunyizia mazao maji; kwanza,Mto Nile na mabaki yake yalikuwa chanzo cha maji kwa asilimia kubwa ya kilimo cha unyunyuziaji, na Blue Nile nayo pia ilitumika.Pili mtiririko wa maji kwa mvutoulikuwa njia kuu ya umwagiliaji na tatu sehemu ya eneo la unyunyusiaji ilitumia pampu.

Maji ya Mto Nile nchini Sudan yamekuwa yakitumikakwa karne kwa ajili ya unyunyuziajiwa mimea maji.

Ukame ulioathiri Sudan katika miaka ya 1980 ulikuwa maafa ya asili ambayo yalikuwa na athari za kusagwa kwa mifumo ya umwagiliaji wa nchi. Kufikia miaka ya 1990, mradi mkubwa wa umwagiliaji wa mimea maji ulianzishwa juu ya ardhi kati ya mito ya Blue na White Nile kusini mwa makutano yao huko Khartoum .

Sudan Kusini imepata uhuru wakati wa mabadiliko ya mapinduzi ambayo yamefanyika katika fedha na uchumi, teknolojia na hata utawala. Sudan Kusini imeamua kuchukua faida ya mifumo iliyojaribiwa ili kuendeleza uchumi wake katika sekta kama vile utalii, makazi, fedha, kilimo kati ya wengine.

Sekta ya kilimo, kama sekta nyingi nchini Sudan Kusini, inahitaji kiwango cha juu cha uwekezaji. Mapema miaka ya 1990, kilimo na uzalishaji wa mifugo ulikuwa vyanzo vikuu vya maisha Sudan. Sasa, sekta hii ya kilimo inaajiri takriban 80% ya watu milioni 8.2.

Uhifadhi wa mafuta ya Kusini mwa Sudan unachangia pakubwa kwa mapato ya nchi. Hata hivyo, biashara ya mafuta peke yake haitasaidia uchumi wa Sudan

Kusini. Kuna haja ya kuendeleza Sekta za binafsi zenye ushindani ili kusaidia maendeleo ya Sudan Kusini.

Sudan Kusini ina rasilimali nzuri za asili kwa ajili ya uzalishajiwa mazao mbalimbali ya mimea, ya umwagiliaji na ya mvua, misitu, uvuvi na mifugo.Lakini rasilimali hizi hazitumiki kwa  kiwango chake ,kwa mfano,Kwa sasa nchi hii inauza bidhaa nyingi na mazao ya kilimo safi kama vile mboga kutoka majirani zake. Mji wa Juba kwa mfano, vifaa vyake vingi vinatoka Uganda. Hii huja kwa bei kubwa na inaweza  kuwa na hatari kwa mfano; uharibifu wowote katika mchakato wa kuagiza, kama vile ,kuvunjika kwa miundombinu au mavuno ya chini ya mazao nchini Uganda, inaweza kusababisha mgogoro wa chakula Sudan Kusini . Ni vizuri nchi ya Sudan Kusini ijisimamie na Kupanua uchumi wake kupitia uwekezaji katika kilimo.

Kupitia uwekezaji katika kilimo, Sudan Kusini inaweza kuongeza maendeleo yake yote na kuunda nafasi ya ajira pamoja na kuboresha chakula .Taifa hii ikijikakamua katika uwekezaji na biashara pia itakuwa imewekwa kwa ushirikiano kati ya sekta binafsi na za umma. Kuimarisha uwekezaji wa sekta binafsi katika kilimo kutapunguza kukua kwa umaskini kwa kuongeza nafasi ya ajira.

## MASWALI

1. Kulingana na kifungu unyunyuziaji wa mazao ulianza lini?
2. Orodhesha njia tatu zilizotumika katika unyunyuziaji mimea maji
3. Ni mito ipi ambayo imesaidia katika kilimo cha sudan kusini?
4. Njia za unyunyiziaji maji zIliathiriwa na nini?
5. Sudan Kusini imeamua kujiendeleza katika nyanja mbalimbali.Taja nne za nyanja hizi.
6. Kilimo cha taifa la Sudan Kusini kilichotajika katika miaka ya 1990 ni kipi?
7. Kilimo hiki kina manufaa gani?
8. Taja biashara nyingine ambayo inainua uchumi wa sudan Kusini.

9. Taifa la Sudan Kusini bado linategemea nchi zingine kwa ustawi wake.thibisha kulingana na kifungu.
10. Sekta za kibinafsi katika kilimo zitasaidia ukuaji wa uchumi wa Sudan Kusini. Thibitisha kulingana na kifungu.

**KIFUNGU C**

## KILIMO CHA MPUNGA

Mpunga nimmea wa pili la chakula kwa umuhimu unaolimwa sehemu nyingi. Umuhimu wammea huuumejitokeza kutokana na jamii za mijini na vijijini kupendelea zaidi kula wali na kupunguza ulaji wa vyakula vingine na kulifanya zao hili kuwa la chakula na biashara.

Ili mpunga uweze kuzaa vizuri unahitaji maji.Mvua ni chanzo kikuu cha maji kwenye kilimo cha mpunga. Viwango vya mahitaji ya maji katika kukua kwa mpunga hutofautiana miongoni mwa aina za mpunga. Ni kwa jinsi hii mpunga hupandwa katika mazingira mbalimbali kutegemea mahitaji yake ya maji. Zipo aina tatu kuu za mazingira yanayolimwa mpunga kulingana na upatikanaji wa maji na hali ya mwinuko wa nchi. Mazingira haya ni kilimo cha mpunga wa mabondeni kinachotegemea mvua ya asilimia 72%. Pili ni kilimo cha mpunga wa kwenye miinuko kinachotegemea mvua ya asilimia 20% na tatu ni kilimo cha mpunga cha umwagiliaji kinachotegemea mvua ya asilimia 8%.

Kiasi cha mpunga kinachozalishwa nchini huongezeka katika eneo linalolimwa mpunga kutokana na kuongezeka kwa miradi midogo ya umwagiliaji pamoja na matumizi ya teknolojia bora za kilimo.



Shamba la mpunga

Katika maandalizi ya mashamba ya mpunga, ni vyema mashamba yaandaliwe mapema kabla ya msimu wa kupanda haujaanza ili kumpa mkulima fursa ya kupanda kwa wakati unaotakiwa. Kuna njia mbalimbali zinazotumika kuandaa mashamba. Kati ya njia hizi ni pamoja na kufyeka, kung'oa visiki na kulima. Shamba linaweza kulimwa kwa kutumia jembe la mkono ambalo wengi hutumia, jembe la kukokotwa na wanyama kama ng'ombe au matrekta.

Baada ya kulima, shamba huwekwa maji ili liloane vizuri na kisha udongo unachanganywa vizuri na maji ili kutengeneza tope. Mbinu hii inarahisisha kupandikiza miche na kuhifadhi maji.

Matumizi ya mbegu bora ni muhimu katika upatikanaji wa mavuno mengi na bora. Kuna makundi mawili makuu ya mbegu ambayo nimbegu za asili za mpunga nambegu zilizoboreshwa. Mbegu za asili za mpunga ni zile ambazo zimetumika miaka mingi katika historia ya kilimo. Wakulima wanazipenda

mbegu hizi kutokana na kuwa na sifa kama vile ladha nzuri, uvumilivu wa matatizo mbalimbali ya kimazingira na kwa sababu ya uwezo wa mbegu hizi kustahimili katika hali mbaya ya hewa na hazihitaji uangalizi wa hali ya juu.Sifa hizi ni matokeo ya mbegu kumudu mazingira na uchaguzi wa mbegu uliofanywa na wakulima kwa miaka mingi. Hata hivyo, nyingi ya mbegu hizi zina uwezo mdogo wa kuzaa, zinachelewa kukomaa, ni ndefu na rahisi kuanguka.

Mbegu zilizoboreshwani zile zilizoboreshwa kutokana na mbegu za asili. Zinazaa sana hasa kwa kilimo cha umwagiliaji. Hata hivyo, hazikidhi ladha ya walaji, ukoboakaji wake si mzuri na baadhi hazistahimili kwenye mazingira mengi ya kawaida. Hii imezifanya mbegu hizi kukubalika na wakulima kwa kiwango kidogo sana.

Mbolea ya kupandia mpunga inahitaji utaalamu wa aina yake. Viwango vya mbolea ya kupandia mpunga hutajika kupimika kulingana na maelezo ya wataalamu.

Kuna njia mbili kuu zinazotumika kupanda mpunga shambani. Njia hizo ni ile ya kupanda mbegu moja kwa moja shambani na ile ya kupandikiza miche.Njia yaKupanda mbegu moja kwa moja hutumika kwenye shamba lililotayarishwa vizuri. Njia ya kawaida waitumiayo wakulima ni ile ya kumwaga na kufukia mbegu. Njia zingine ni zile za kupanda mbegu kwenye mashimo yaliyo kwenye mstari na kwa kuzingatia nafasi maalum au mbegu hupandwa kwenye mashimo bila kufuata mstari na bila kuzingatia nafasi iliyopendekezwa. Vile vile mbegu hupandwa kwa kunyunyizwa kwenye vifereji vyenye vina vifupi na kufukiwa pasipo kuwa na nafasi maalum kati ya punje na punje.

Njia ya kupandikiza miche hutumika kwa kupanda mbegu kwanza kwenye kitalu kabla ya kuzihamishia shambani. Mara nyingi mbegu hizi hutumia wiki tatu hadi nne baada ya kuota kwenye kitalu na kufikia umri wa kupandwa shambani. Katika shamba la mpunga miche hupandwa shambani kwenye mstari na kwa nafasi maalum au kupandwa kiholela bila kuzingatia nafasi maalum za kupanda.

Mkulima anashauriwa kupanda miche katika kina cha sentimeta 2 hadi 3. Kuna hatari ya kupanda kina kirefu kwa vile machipukizi huchelewa kujitokeza. Baada ya kupandikiza miche, machipukizi hujitokeza baada ya siku 5 hadi 10.



**Kupandikiza miche ya mpunga**

Kupanda kwa nafasi ni kati ya njia bora za kilimo inayomwezesha mkulima kupata mazao bora. Hivyo ni muhimu sana kuzingatia kupanda kwa mistari na kufuata nafasi zinazoshauriwa na wataalamu wa kilimo.Muda wa kupanda unatofautiana kutoka eneo moja kwenda jingine kulingana na majira ya mvua.

Ni muhimu shamba lipaliliwe ili kuondoa magugu. Magugu ni mimea hivyo hushindana na mimea iliyopandwa na mkulima kwa kunyonya virutubisho ardhini. Magugu yanaweza pia kuhifadhi wadudu na magonjwa yanayoweza kushambulia mimea iliyopandwa na hivyo kupunguza mavuno.

Ni vizuri katika kilimo cha mpunga, shamba lipaliliwe mara mbili, kutegemeana na hali ya magugu katika shamba. Unaweza kupalilia kwa kung’olea kwa mkono, kwa mashine au kwa kutumia dawa ya kuua magugu. Shamba la mpunga

ambalo halijapaliliwa linaweza kupunguza mavuno kwa asilimia kubwa ya mavuno yanayotarajiwa.



Shamba la mpunga uliopandwa kwa mistari



**Uvunaji wa mpunga**

Baada ya kuuvuna mpunga, njia za kukausha ni kwa kuurundika pahali pakavu halafu kuupigapiga ili kutenganisha masuke na mpunga. Kama mpunga haujakauka vizuri hukaushwa zaidi juani ili kupunguza unyevunyevu kufikia kiwango kinachofaa kwa kuhifadhi. Ni muhimu mpunga ukauke vizuri ili usioze ukiwekwa ghalani.Mpunga safi huwekwa kwenye gunia na magunia kupangwa vizuri ghalani juu ya mbao yasiguse sakafu.

## MASWALI

1. Taja sababu za watu wengi kupanda mpunga.
2. Ni nini umuhimu wa maji kwa mpunga?
3. Taja mazingara matatu ambayo yanawezesha upandaji wa mpunga.
4. Taja njia mbili zinazoongezea uzalishaji wa mpunga.
5. Ni shughuli zipi za awali ambazo mkulima anapaswa kufanya ili kuandaa shamba la mpunga?
6. Taja vifaa vitatu vya kulima shamba la mpunga.
7. Mbinu ya kuchanganya mchanga na maji ina umuhimu gani?
8. Tofautisha:i) Mbegu za asili na ii)mbegu zilizoboreshwa.
9. Orodhesha sifa nne za mbegu za asili.
10. Fafanua changamoto tatu za mbegu za asili.
11. Mbolea hutumikaje katika upanzi wa mpunga?
12. Kuna njia tatu za kupanda mpunga.Zitaje.
13. Mbegu huchukua muda gani kuota baada ya kupandikizwa kitaluni?
14. Upandaji wa kupanda miche kwenye shamba hufanywaje?
15. Kwa nini mkulima anashauriwa kutotumia mashimo mapana ya kupanda?
16. Taja njia tatu unaweza kutumia kupalilia mpunga.
17. Taja madhara ya magugu.
18. Eleza umuhimu wa kupalilia mpunga.
19. Mpunga unanadhifishwaje ili kutolewa masuke?
20. Eleza huhifadhi mzuri wa mpunga.

**KIFUNGU D**

## UFUGAJI MSETO



Ufugaji mseto ni hali ya kufuga aina mbalimbali za wanyama au miti,mboga kwa pamoja. Kwa mfano mkulima anaweza kufuga wanyama mbalimbali kama kondoo,mbuzi na ng'ombe pamoja.Ufugaji mseto unafanyika kwa mfano iwapo shamba ni dogo mfumo wa ufugaji mseto hufaa sana.

Ufugaji mseto wa samaki ni ufugaji ambao bwawa la samaki linakuwa ndani ya shamba pamoja na shughuli nyingine za shamba aidha hapo hapo shambani au katika eneo lililo mbali kidogo na shamba. Shughuli za shamba zinazoenda sambamba na ufugaji wa samaki ni pamoja na kilimo cha mazao mbalimbali kama vile mboga , mpunga na kadhalika au ufugaji wa wanyama mbalimbali kama vile kuku, ng'ombe, mbuzi na kadhalika.

Kuna baadhi ya mambo ya kuzingatia kabla ya kuanza ufugaji mseto wa samaki.Inabidi mkulima ajiulize kiasi anachotaka kuwekeza katika mradi, kiasi cha pesa pamoja na nguvu kazi atakazotumia kutoa huduma kwenye mabwawa

ukilinganisha na shughuli zingine za shamba na sababu ya kufuga samaki. Pia katika ufugaji mseto wa wanyama na samaki, aina ya wanyama inabidi izingatie imani ya kidini katika eneo husika la ufugaji na walaji. Pia inabidi mfugaji azingatie suala la upatikanaji wa vyakula vya mifugo.

Kufuga samaki pamoja na shughuli nyingine za shamba kuna faida nyingi kama vile;kunaongeza ufanisi, huongeza mavuno na hatimaye faida inayopatikana inakuwa kubwa.Kunakuwa na matumizi mazuri ya eneo la shamba, mazao ya kilimo ama mabaki yake hayapotei bali yanatumika katika kulishia samaki. Kuna aina kadhaa za ufugaji mseto wa samaki, kwanza niUfugaji mseto wa kilimo cha mazao na samaki: Mimea inayolimwa mashambani au isiyolimwa yaweza kutumika kama chakula cha samaki au kutengenezea chakula cha samaki. Mimea hii pia yaweza kutumika kama mbolea ya kurutubisha shamba hasa pale ambapo mbolea ya wanyama ni nadra kupatikana. Mimea ambayo imekuwa ikitumika katika maeneo mengi kama chakula cha samaki ni pamoja na majani tembo, mahindi, viazi vitamu, mtama, maharage ya soya, mboga kama mchicha, sukuma wiki na spinachi.Mabaki ya mazao yatokanayo na mimea kama vile mihogo, maganda ya ndizi, majani ya mapapai na maganda yake, pumba za mahindi, mtama, ufuta na mpunga hutumika kama chakula cha samaki. Kama eneo linafaa kwa kilimo cha mpunga basi mkulima anaweza kutengeneza mseto wa mpunga na samaki.

Aina ya pili ni mseto wa kuku au bata na samaki.Wakulima wengi huwa wanafuga kuku au bata katika maeneo yao ya kuishi. Faida au mazao yatokanayo na kuku ni pamoja na mayai, nyama na kinyesi cha kuku. Kinyesi cha kuku kina virutubisho vingi kwa matumizi ya shamba pamoja na mabwawa ya samaki. Katika mseto huu banda la kuku au bata linaweza kujengwa kando ya bwawa au juu ya bwawa la samaki. Katika mseto wa bata na samaki, huwa bata anatumia bwawa kama sehemu ya kuishi na malisho wakati huo akiwa anarutubisha bwawa. Bata huwa wakati wa mchana anatafuta chakula ndani ya bwawa na usiku anakuwa kwenye banda. Bata huwa wanakula viluwiluwi wa Chura,

vimelea vya mbu, wadudu na majani ambayo yamo ndani ya bwawa.
Aina ya tatu ni   mseto wa ng'ombe, mbuzi, kondoo au sungura na samaki. Tofauti na kuku au bata, mbolea itokanayo na samadi cha wanyama kama ng'ombe, mbuzi na kondoo huwa ina virutubisho vichache. Hata hivyo hii mbolea inaweza kutumika baada ya kuikusanya kwa muda kabla ya kuitumia. Rojorojo itokanayo nasamadi ya ng'ombe baada ya kupitia kwenye mtambo wa biogesi ni nzuri zaidi kutumika katika mabwawa ya samaki. Mbuzi na kondoo wanaweza kutumiwa ingawa katika maeneo mengi ni vigumu kukusanya kinyesi chao kutokana na mfumo wa ulishaji. Kinyesi cha sungura pia kinaweza kutumika katika kurutubisha bwawa kwa kujenga banda juu ya bwawa kama ilivyo kwa upande wa ufugaji kuku.

Sio samaki wote wanafaa katika kilimo mseto.Aina ya samaki wanaofaa katika kilimo mseto hutegemea mahali mbalimbali.Kuna mahali ambako aina ya samaki wa Perege na Kambare ndio wanaofugwa. Perege ndiye ambaye anafahamika zaidi kwa wafugaji. Chakula cha asili cha perege ni vimelea vya kijani vilivyomo ndani ya maji lakini ana uwezo wa kula aina nyingi za vyakula ikiwa ni pamoja na pumba za mahindi na mpunga, majani na mabaki ya jikoni. Vile vile anakua vizuri kama kutakuwa na mbolea ya samadi na ya chumvi chumvi, na anaweza kuhimili kiasi kidogo cha hewa ya oksijeni. Madume ya Perege hukua haraka zaidi kuliko majike, na uvunaji unaweza kufanyika baada ya kufikisha uzito wa gramu 250. Kambale hula vyakula vya asili ndani ya maji kama vile wadudu, konokono, viluwiluwi wa chura na samaki wengine wadogo. Vile vile anakula vyakula vya ziada kama vile mabaki ya vyakula hasa yenye asili ya nyama. Kambale hutumika kupunguza wingi wa Perege ndani ya bwawa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Perege anazaliana kwa wingi kwenye bwawa. Kambale anakua haraka sana kama chakula chenye protini kinapatikana kwa wingi. Kambale anaweza kuishi kwenye maji yenye hewa kidogo ya oksijeni. Tofauti na Perege, Kambale ana mifupa michache na minofu mingi na ni mtamu hasa anapokaushwa kwa moshi.

Mboga zinafaida katika ufugaji mseto wa samaki kwa sababu ni chanzo cha chakula cha samaki. Jamii ya samaki wengi wanaofugwa niwale wanaokula majani hivyo mabaki ya mboga kutoka bustani hukatwa katwa vipande vidogo vidogo kwa ajili ya kulisha samaki.

Ufugaji mseto wa samaki wa bustani hulenga kuwa kitega uchumi kikubwa kwa wakulima wadogo. Mavuno ya mazao ya bustani huuzwa kirahisi kwa kuwa yanahitajika kwa wingi na jamii kutokana na umuhimu wake. Fedha inayopatikana husaidia katika utunzaji wa shamba mseto ama kutumika katika mahitaji mengine ndani ya familia ya mfugaji.

Mboga hutumika kama mbolea kwenye bwawa la samaki. Mboga huozeshwaili kutoa mimea na wadudu wa asili ambao hutumika kama chakula cha samaki. Hii hupunguza gharama za uzalishaji kwenye bwawa la samaki.

## MASWALI

1. Ufugaji mseto ni nini?
2. Ufugaji mseto una tokea kwa sababu gani kulingana na kifungu?
3. Eleza mbinu ya ufugaji samaki mseto.
4. Taja mambo matano ya kuzingatia kabla ya kuanzisha mradi wa ufugaji mseto wa samaki.
5. Orodhesha faida nne za kufuga samaki pamoja na shughuli za shamba.
6. Taja aina tatu za ufugaji mseto wa samaki.
7. Ni zipi faida za mimea kwa samaki?
8. Eleza umuhimu wakinyesi cha kuku.
9. Bata anapelekea samaki faida gani?
10. Kwa nini faida ya smadi ng’ombe ni tofauti na kuku kwa samaki?
11. Eleza kinachozingatiwa katika uchaguzi wa samaki wa kufuga mseto.

12. Samaki aina ya perege ana manufaa mengi ya kufuga mseto kuliko kambale.Yataje manufaa haya.
13. Samaki aina ya kambale hula nini?
14. Orodhesha sifa nne za kambale.
15. Mboga iliyooza ina manufaa gani kwa samaki?
16. Ufugaji mseto wa samaki na mboga una manufaa yoyote kwa mkulima?
17. Ni mbinu ipi inatumika kupatia samaki kinyesi cha sungura?
18. Chakula cha bata ni kipi kwenye bwawa la samaki?
19. Taja ufugaji mseto unaondelezwa katika jamii yako.
20. Je, kulinganana wewe ufugajimseto una manufaa yoyote?

**KIFUNGU E**

## UHANDISI JENI (GMO)



Mahindi yaliyozalishwa kwa teknolojia ya GMO.

Uhandisijeni ni teknolojia ambayo hubadilisha mmea au mnyama kwa njia ya teknolojia ya kuchanganya jenetiki yaani DNA (chembe hai) za mmea au mnyama mmoja na mwingine tofauti, ili kuupa mmea huo mpya au mnyama huyo mpya tabia zisizo za asili.

Uzuri wa teknolojia ya GMO ni kwamba inaweza kumsaidia mkulima kuvuna mazao mengi katika eneo dogo, kutotumia au kutumia kidogo dawa za kuulia wadudu na mazao kumea vyema kwenye maeneo yenye mvua kidogo.

Kwa mfano, mimea inayoota baharini, kwenye chumvi au katika miamba hufanyiwa utafiti wa kimaabara na hivyo jeni zake huchukuliwa na kuwekwa katika mimea mingine.Teknolojia hii hutafuta sifa iliyo katika mmea mmoja na kuipandikiza katika mmea mwingine ili kuhamisha sifa hizo.

madhumuni ya kutumia teknolojia ya uhandisi jeni ni kupambana na changamoto za magonjwa, ukame na mabadiliko ya tabianchi.Sababu kubwa ya kutumia teknolojia hii ni kulinda usalama wa chakula kwani mkulima huwa na uhakika wa kupata mazao mengi na pia mazao yenye afya.

Mazao ya GMO yaliyoingia sokoni mpaka sasa ni soya, pamba, canola na mahindi huku nchi za Afrika ambazo tayari zimeanza kuvuna mazao ya GMO ni Afrika Kusini, Burkina Faso, Misri na Sudan.

Katika kufafanua umuhimu na changamoto za kilimo za mazao ya GMO bado kuna wasiwasi miongoni mwa wanajamii kuhusu athari zinazoweza kupatikana kutokana na teknolojia hii licha ya kuwapo kwa miongozo na mfumo wa usimamizi wa matumizi salama ya teknolojia hiyo.Hata hivyo, mikakati imeweka katika kushughulikia masuala ya matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa.Wananchi wanapewe elimu ya kutosha kuhusu mazao ya GMO hasa kwa kuangalia sera, sheria, mfumo na kanuni zilizowekwa za bioteknolojia.

Nchi mbalimbali zimekuwa zikitamani kuona wananchi wake wanazalisha vyakula vya kutosha, pengine kuwa na ziada kwa ajili ya kuuza, lakini zimekuwa na hofu ya kujiingiza kwa kuwa hii ni teknolojia mpya. Kuna maswali mengi ikiwa GMO ina madhara. Wataalamu mbalimbali wamekuwa wakisema kuwa mazao yanayopatikana kwa teknolojia hii hayana madhara, baada ya kufanya tafiti mbalimbali.

Hata hivyo, baadhi ya wataalamu na wanaharakati wamekuwa wakibashiri kuwa huenda mazao ya namna hiyo yakasababisha athari za kimwili na mazingira. Pamoja na kauli hizo hakuna hata mmoja ambaye amekuja na uthibitisho wa kisayansi.

Umoja wa Ulaya (AU) umetoa ripoti yao inayojumuisha miradi ya utafiti zaidi ya 130 yenye lengo la kutathmini madhara ya uhandisi jeni.Ripoti hiyo ilijiridhisha kuwa mazao ya chakula yaliyolimwa kwa teknolojia ya uhandisi jeni hayana madhara ukilinganisha na mazao ya kawaida.

## MASWALI

1. Eleza maana ya uhandisi jeni.
2. Uhandisi jeni unabadilishi mmea au mnyama vipi?
3. Taja manufaa matatu ya uhandisi jeni kwamkulima.
4. Toa sababu za mmea kupandikizwa kwenye mmea mwingine.
5. Ni sababu gani inayofanya mimea iliyoko kando ya bahari kupandikizwa kwa mingine?
6. Orodhesha mazao ambayo tayari yamepatikana kutokana na uhandisi jeni.
7. Taja nchi ambazo zimenufaika na teknolojia hii.
8. Ni mikakati ipi ambayo imewekwa ili kuondoa wasiwasi wa matumizi ya teknolojia miongoni mwa Wananchi?
9. Toa sababu ya nchi zingine kutotaka watu wake kutumia teknolojia hii.
10. Ripoti ya Umoja wa Ulaya ilitoa ripoti gani kuhusiana na teknolojia hii?

## Mada Ndogo ya 3: Sarufi

### HALI

Kuna hali mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Hali huwakilishwa na viambishi. Viambishi vinavyowakilisha hali havionyseshi wakati maalum wa kutendeka. Viambishi hivi huonyesha kitendo hufanyika katika hali fulani. Huweza kuonyesha kama kitendo hufanyika mara kw mara, masharti ya kutendeka kwake, n.k. Viambishi hivi ni kama **me** na **hu**.

**Hali timilifu (me)**

Hali hii huwakilishwa na kiambishi **me** katika sentensi. Hali hii hutumiwa kuonyesha kuwa kitendo kinachozungumziwa tayari kimetendeka lakini si muda mrefu uliopita.

***Mifano:***

1. Sweta yake i**me**raruka.
2. Jembe jipya li**me**nunuliwa.
3. Mwalimu a**me**fika darasani.
4. Wanafunzi wengi wa**me**lipenda somo la Kiswahili.
5. Mkulima a**me**palilia mahindi.

### Zoezi

**Geuza sentensi hizi ziwe katika hali timilifu.**

1. Tulikula chakula kitamu.
2. Mvuvi alitega samaki wengi.
3. Mwalimu aliwaadhibu wanafunzi.
4. Wazazi walihudhuria mkutano shuleni.
5. Raia walitii sharia.

6. Mwanafunzi ngonjwa aliruhusiwa kwenda nyumbani.
7. Wachoraji walimaliza kuichora picha nzuri.
8. Mama alifua nguo.
9. Sisi tulienda mtoni kuteka maji.
10. Wao walicheza kandanda.

## Hali ya mazoea (hu)

Kiambishi hu hutumiwa kuonyesha hali ya mazoea. Mazoea hurejelea hali ya kukifanya kitu au jambo mara nyingi hadi ikawa sehemu ya tabia ya mtu.

***Mifano:***

1. Mtoto hunywa maziwa.
2. Mwalimu husahihisha vitabu.
3. Sisi huenda shuleni asubuhi na mapema.
4. Wao huchora picha nzuri.
5. Wazazi hulipa karo ya shule.

## Zoezi

**Geuza sentensi zifuatazo katika hali ya mazoea.**

1. Mama anapika chakula.
2. Mtoto anandika kitabuni.
3. Wasichana wameenda mtoni.
4. Mwalimu anaandika kwenye ubao.
5. Sisi tunalinda ng’ombe.
6. Wao watafanya mtihani.
7. Sisi tutashiriki mashindano ya kandanda.
8. Seremala ametengeneza meza nzuri.
9. Wanafunzi waliomba darasani.
10. Daktari anamtibu mgonjwa.

## Mada Ndogo ya 4: Kuandika

1. Andika kifungu juu ya umuhimu wa kilimo nchini mwenu.
2. Matumizi ya dawa za kunyunyuzia mimea ni hatari. Jadili
3. Umealikwa kuwahutubia wakulima juu ya kilimo bora. Andika hotuba yako.

## Mada Ndogo ya 5: **Msamiati**

Msamiati wa mimea: Mboga na Matunda



kabichi



Vitunguu



Pilipili Hoho



Viazi



Dania



Nyanya



Karoti



Sukuma wiki




| **Mmea** | **Zao** |
|---|---|
| 1. Mpunga | mchele |
| 2. Mfenesi | fenesi |
| 3. Mzabibu | zabibu |
| 4. Mchungwa | chungwa |
| 5. Mpera | Pera |
| 6. Mtikiti | tikiti |
| 7. Mkwaju | kwaju |
| 8. Mnazi | nazi |
| 9. Mtomoko | Tomoko |
| 10. Mchikichi | chikichi |
| 11. Mbuni/ mkahawa | kahawa |
| 12. Mpapai | papai |
| 13. Mtufaha | tufaha |
| 14. Mwembe | embe |
| 15. Mtangawizi | tangawizi |
| 16. Mkabichi | kabichi |
| 17. Mkuyu | kuyu |

**Zoezi**

1. Mkiwa kwa makundi ya wawili wawili, jadilianeni majina ya matunda mliopewa.
2. Wewe na mwenzako, someaneni majina ya mboga mnazonunua sokoni.

**SURA YA 3**

# MITINDO YA MAVAZI YA KIAFRIKA

**Mada Ndogo ya 1:** Kusikiliza na kuzungumza

MAVAZI YA WANAWAKE

Natembea natazama, ni hali ya kushangaza,
Mitaani akina mama, mambo wanayoigiza,
Wengine watuwazima, inakuwaje nawaza,
Mavazi mnayovaa, ya aibu kinamama.

Vazi la Mwanamke, tangu kale heshima,
Watu walijivunia, wa rika zote nasema,
Haya nawasimulia, walivaa akina mama,
Mavazi mnayovaa, ya aibu kinamama.

Suruali mwavalia, mfanane na wazungu,
Asili mwaikimbia, mnanitia uchungu,
Watu wote angalia, mnamdharau Mungu,
Mavazi mnayovaa, ya aibu kinamama.

Vimini mwajibalia, mwana kama vikatuni,
Nyingine mnapasua, makusudi mapajani,
Mapaja twaangalia, pia na nguo za ndani,
Mavazi mnayovaa, ya aibu kinamama.

Siketi taiti pia, mitaani mwavalia,
Hiyoni ya kulalia, maungo yaoneshea,
Mitaani mwatembea, watu kwa kuangalia,
Mavazi mnayovaa, ya aibu kinamama.

Kweli mwatia karaha, moyoni nasononeka,
Singerendi mwavalia, maziwa yanaonekana,
Mitaani mnahaha, kutwa nzima mwazunguka,
Mavazi mnayovaa, ya aibu kinamama.

Kwa umbo mmeumbika, kwa uzuri asilia,
Uarabu mwautaka, tena kwa kujichubua,
Kama Mungu angetaka, mngekuwa Saudia,
Mavazi mnayovaa, ya aibu kinamama.

Wengine watu wazima, tena ni wake za watu,
Watoto wenu lazima, watawaigeni tu,
Malazi yao lazima yatakuwa yenye kutu,
Mavazi mnayovaa, ya aibu kinamama.

Hapa mimi nasimama, naomba mnisikie,
Wanamama wenye hekima, hali hii tukemee,
Hakika mimi nasema, tena isiendelee,
Mavazi mnayovaa, ya aibu kinamama.

## MASWALI

1. Taja dhamira ya mwandishi katika shairi hili.
2. Mshairi analalamikia nini katika ubeti wa 4?
3. Ni mavazi yepi yanayolengwa katika ubeti wa 5?

4. Mavazi yanayotajwa katika ubeti wa tano yamefanyiwa madhara gani?
5. Madhara katika mavazi ubeti wa 5 yanasababisha aibu zipi?
6. Kulingana na mshairi ni nini nia ya wanawake kuvaa siketi taiti?
7. Eleza maana ya ‘’Singerendi mwavalia, maziwa yanaonekana’’.
8. Eleza ubeti wa 8 kwa lugha ya kawaida.
9. Ni athari gani ambayo mtoto anapata kutoka kwa mama?
10. Mshairi anawashauri kina mama wasiovaa vibaya wafanye nini?

## Mada Ndogo ya 2: Kusoma

**KIFUNGU A**

### MAVAZI YA KIAFRIKA



Kutoka zama za kale hadi mwanzoni mwa karne ya 19 kabla ya kuja kwa wazungu waafrika walikuwa na utamaduni wao;mfumo wa jinsi ya kuishi uliojumuisha lugha,ibada na mavazi.Mambo ya teknolojia katika karne hizo ilikuwa chini sana ukilinganisha na mabara mengine yaliyoendelea kama Ulaya na Amerika. Hata hivyo,historia inatuonyesha kuwa wazee wetu walikuwa na ubunifu wa hali ya juu wa kutumia mazingira yao kuweza kujitengenezea vitu mbalimbali zikiwemo zana za kilimo ,uwindaji,uvuvi,kupikia na hata

utengenezaji wa mavazi yao. Hata katika uchanga huu wa teknolojia waafrika waliweza kujitengenezea mavazi ya kuweza kujisitiri -*mavazi ya kiafrika*. Mavazi ya Waafrika Kabla ya Uvamizi wa Wageni ni kuwa waafrika walikuwa wakitengeneza mavazi yao na kujivika kutoka kwa ngozi za wanyama waliokuwa wakiwawinda na magome ya miti ambayo yalilainishwa na kuwa kama nguo laini.Walijivika maungo yao hasa sehemu za siri. Hii inaonyesha kuwa kuvaa kwa kuficha sehemu fulani muhimu mwilini ni utamaduni wa toka zama za mababu zetu. Hii inaweza ikaonekana hata leo katika baadhi ya makabila kama Wamaasai.Hata katika uhaba wao wa teknolojia waliweza kujitengenezea mavazi ya kusitiri mwili.

Wageni walipovamia Afrika kwa ajili ya biashara na kutafuta malighafi walikuja na tamaduni zao mpya zikiwemo za mavazi.Waarabu na Wazungu walikuwa wameendelea zaidi kiteknolojia katika karne hii na walihitaji malighafi kwa ajili ya viwanda vyao vya nguo huko kwao na Afrika kulikuwa ni sehemu muafaka kwa hilo.Kwa kuwa nguo zao zilitengenezwa na mashine za hali ya juu kuliko zile za Afrika,Waafrika wakaanza kuvaa nguo za nje zaidi kuliko za kwao. Hapa ndipo kutawaliwa kwa mavazi kulipoanzia.Walileta nguo na urembo mwingine na sisi tuliwapa ardhi na madini yetu.

| | |
|---|---|
| <br>*Vazi la Mama wa Kiafrika na Mtoto Nyakati za Uvamizi wa Wazungu* | <br>*Aina ya Vazi na Urembo wa Mwanamke wa Kiafrika katika Karne ya 19* |
| <br>*Vazi la Wanawake katika Siku Maalumu* | <br>*Vazi la Kiongozi wa Kiafrika-Chifu* |

Wazungu walizibagua sana tamaduni za kiafrika na kuziita za kishenzi,na kupenyeza tamaduni za kwao yakiwemo mavazi.Waafrika wakaanza kuvaa suruali na suti za kizungu. Wanawake nao wakaanza kuvaa suruali, hii pia nia athari ya Wazungu.  Kwa kuwa Wazungu waliwafanya Waafrika wafikiri kuwa kila kitu cha kwao ni kizuri namna ya uvaaji wa wafrika na maadili ya mavazi yao yakaanza kufifia.

Leo hii mavazi ya kiafrika yanavaliwa katika matukio maalumu tu na sio katika maisha ya kila siku ya nyumbani ama ofisini. Tunavaa mavazi ya asili katika sherehe za harusi au za kuwaaga wali.Baadhi ya mavazi leo yanaenda kinyume na maadili ya kiafrika. Kama tulivyoona hapo mwanzo kuwa wazee wetu katika umasikini wao wa teknolojia waliweza kuvaa mavazi kwa nia ya kufunika maungo yao,lakini leo hii katika maendeleo makubwa ya teknolojia ya utengenezaji mavazi ,watu wanavaa mavazi yasiyo na staha yenye kuacha miili yao nje. Mavazi haya hayaendani na asili ya Waafrika.

Kuna mitindo mingi tu ya asili ya Afrika ambayo ni mizuri na yenye staha. Mavazi haya yanapendwa hata na wazungu wenyewe ambao tunafikiri kila kitu chao ni kizuri.Hii hapa ni baadhi ya mitindo lukuki ya kisasa ambayo ina asili ya Afrika na inavutia. Mingi ni ya kike kwani wanawake ndio wenye aina nyingi za mavazi.

**a) Mitindo ya mavazi ya Wanawake**





| | |
|---|---|
|  |  |
|  |  |

**b) Mitindo ya mavazi ya Wanaume**

| | |
|---|---|
|  |  |










Mitindo anuwai ya mavazi ya Kiafrika yenye rangi za kuvutia imesababisha wabunifu wengi wa nchi za kigeni kuwa na hamu ya mavazi ya kiafrika.Hii imewapa msukumo wa kuagiza vitambaa na rangi kutoka bara la Afrika. Nchi hizi za kigeni hunufaika pakubwa na biashara ya nguo kutoka bara la Afrika hasa katika miezi ya majira ya joto.Wakati kama huu maduka ya rejareja yanafurika na mavazi ya kuongoza ya Kiafrika.Hii ni kwa sababu mavazi haya yanaweza kukinga hali ya hewa na pia kutumika katika msimu au majira ya baridi.

Kwa upande wa utunzaji wa utamaduni, mitindo ya Kiafrika ya mavazi inavutia si haba.Mitindo yake ina una rangi mahiri za kupendeza na zenye sifa

maarufu.Rangi kama hudhurungi, samawati, kijani na wakati mwingine mchanganyiko wa rangi mbalimbali unavutia macho.Mitindo ya mavazi ya Kiafrika humulika mila na utamaduni wa kabila fulani.Hii hupelekea kuzipa mizizi mila natamaduni za watu hawa umaarufu usioweza kuondolewa kwa haraka.

Mojawapo ya vitambaa vingi zaidi katika Afrika vinavyotengeneza nguo za jadi huwa ni Ankara. Ankara ni vitambaa ambavyo hutumia pamba kwa asilimia100% kwa hivyo unadhifu wake ni wa hali ya juu.Vitambaa vya Ankarahutumika kwa kushona aina nyingi za mavazi kama vile nguo, vitambaa vya kichwa, jaketi, kati ya zingine.

Mitindo ya mavazi ya Kiafrika inabadilika kila uchao.Kila wakati soko hujaa mitindo mipya ya mtindo hii,manufaa yalioaje!Hii huchangia uzalishaji wa ujira kwa maana vitambaa avinahitajika kila uchao.Watu wengi hunufaika kwa kufanya kazi kama kutengeneza na kuunganisha vitambaa katika sekta hizi za nguo.

Hata hivyo,kutokana na mabadiliko mengi ulimwenguni kama vile kuongezeka kwa vyombo vya habari vya kijamii, mazingira,teknolojia mitindo wa mavazi ya Kiafrika yamebadilika na mtindo wa Kiafrika umeathiriwa na wabunifu wa kigeni.Matangazo ya biashara yameathiri kwa kiwango kikubwa mitindo hii ya Kiafrika. Ni wakati sasa waafrika waurudie utamaduni wao kwani Afrika kuna vitu vingi vizuri yakiwemo mavazi. Tuutunze na kuuenzi utamaduni wetu kwani ni mzuri na wenye maadili.

**MASWALI**

1. Orodhesha mambo matatu ambayo Mwafrika alikuwa nayo kabla ya kuja kwa mzungu.
2. Je, zama za kale Waafrika walikuwa na teknolojia? Thibitisha kulingana na kifungu.
3. Ni nchi zingine zipi ambazo zilikuwa na teknolojia kuliko Afrika?
4. Zamani Waafrika walipata vyombo vyao kutoka wapi?

5. Taja vyombo vinne ambavyo mababu wetu waliweza kujitengenezea.
6. Eleza ubunifu wa Waafrika katika kujiundia nguo zama za kale.
7. Utamaduni wa Mwaafrika wa kuficha uchi ulianza na mababu zetu.Thibitisha kulingana na kifungu.
8. Ni kabila lipi ambalo badolinathamini utamaduni wa kale wa mavazi kulingana na kifungu?
9. **Taja nia** mbili za wageni kuvamia Bara la Afrika.
10. Kando nakupoteza mavazi yetu, taja vitu vingine viwili tulivyopoteza kwa Wazungu na Waarabu.
11. Katika ulimwengu wa sasa mavazi ya Kiafrika yanatambulika lini?
12. Mavazi ya kisasa yanakiuka utamaduni wa Kiafrika.Thibitisha kwa hoja mbili.
13. Kwa nini mitindo mingi ya Kiafrika ni ya wanawake?
14. Wageni wanavutiwa na nini katika mavazi ya Kiafrika?
15. Toa sababu mbili za wauzaji rejareja wa kigeni kuuza mavazi ya Kiafrika.
16. Ni rangi zipi za nguo zinazohusishwa na Waafrika?
17. Ankara ni nini?
18. Ankara hushona mavazi yepi?
19. Ni vitu vipi ambavyo vimeathiri mavazi ya kiafrika hivi leo?
20. Mwandishi anawahimiza wasomaji nini kuhusu mavazi ya Kiafrika?

**Kifungu b:**

**SHAWISHI ZA SAIZI ZERO ZA UKUBWA**

Ukubwa wa mwili ni kitu ambacho kinatofautiana kwetu sisi sote na ulingana na kujenga kwa maumbo yetu ya kipekee; ushawishi wa saizi zero ukubwa au kwa kiingereza ‘’*Zero size*’’ ni jambo ambalo limeathiriwa kwa kiwango kikubwa na mtazamo wa maumbile ya mtu.

Dhana ya saizi zero ukubwa inazingatia wembamba wa maumbile na kuchukulia kama urembo wa mtu.Kwa Mfano makampuni mengi yanachukulia jambo hili kwa undani kwa mujibu wa kupata ajira katika magazeti ya mtindo. Wao wanawashawishi wanawake wenye umbo jembamba kushiriki maonyesho ya kupigwa picha zinazotumika katika magazeti yao.Picha hizi hutumiwa kama chombo cha kuwanasa watu waweze kununua magazeti haya.

Kwa wasichana wengi saizi zero ni maneno mazuri zaidi na wao wanaweza kufanya jambo lolote ili kupata umbo hilo. Hata hivyo, matokeo ya shinikizo hili ni kamilifu kweli?Je, umefanikiwa kupata kujiangalia wakati wewe ni ngozi tupu iliyoachana na mifupa na unajiita saizi zero ukubwa ? Je, ukubwa wa sifuri ni ukubwa ambao utatufanya tujithamini kama kiumbe mwenye haki zake? Je, utakufa njaa ukitafuta sifa za saizi zero?

Katika utafiti uliofanywa ng'ambo kwa watoto wenye umri wa miaka 8-10, karibu asilimia 50 walisema kwamba hawakuwa na furaha na ukubwa wao. Hii ni shida inayoendelea leo katika jamii. Uchunguzi unaonyesha kwamba idadi ya watoto wanaoingizwa hospitali na matatizo kukataa kula yameongezeka kwa zaidi ya theluthi katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Je, ulimwengu wa mitindo na waandishi wa habari walaumiwe kwa kuunda uvumilivu hatari na kufikia kile kinachodhaniwa kuwa cha ukamilifu?

Siku hizi vyombo vya habari vina ushawishi mkubwa juu ya maoni na uchaguzi wa kila siku: kile tunachovaa; muziki gani tunaosikiliza, kile tunachokula au ikiwa tunachagua kukataa kula kabisa. Ulimwenguwa vyombo vya habari umejaa maonyesho ya nje ya washerehe kama vile wasanii wa vyombo vya habari; watendaji, waimbaji wa nyimbo za burudani au mifano. Katika magazetina majarida ya habari wazo kubwa ni kwamba kupoteza uzito mwingi kutatufanya kusikia furaha.

Hivi karibuni iliripotiwa kwamba kijana mwenye umri wa miaka kumi na mmoja aliteseka kimawazo kutokana na wavulana wengine wa umri wake wote kumcheka kwa sababu ya uzito wake. Watoto wanapotoka kimawazo wanaposoma magazeti na kuangalia matangazo ambayo yanasisitiza kwamba sura nyembamba ni bora. Kwa mfano baada ya kusoma gazeti moja, mvulana mdogo ambaye mara moja alipenda chakula chake alianza kupunguza kalori 1,500 kwa siku ambayo kwa kasi ilipungua hadi 50. Hii ilimwathiri sana kwa sababu watoto wa umri mdogo wanahitaji idadi kubwa ya kalori itakayowafaa katika maisha yao. Ni jambo la kushangaza kwamba vyombo vya habari vinaathiri moja kwa moja maoni ya watoto ya 'kawaida'; hivyo basi, kijana huyu alionekana na wenzake kama mkubwa sana.

Wasichana wanahitajika kufunzwa mwelekeo wa maisha.Umbo la mtu ni kitu cha thamani sana kwa kiwango cha kutoshinikizwa na masuala ya kukonda ili kudai urembo.Tunapaswa kufundisha wasichana tofauti kati ya picha na ukweli.Vitu na picha katika vyombo vya habari vinarembeshwa kwa muda mrefu ili viweze kuonekana maridadi. Pia wasichana wanahitaji kufundishwa ujuzi wa kukataa mambo yanayoathiri umbo lao kwa vyovyote.

Hata hivyo, vyombo vya habari vinapaswa kusaidia kujenga picha nzuri zaidi za mwili na sio kushinikiza watu na picha zao za umaridadi usiokuwa halisi.

## MASWALI

1. Ukubwa wa mwili uandamana na nini?
2. Dhana hii ya saizi zero inazingatia nini?
3. Makampuni yanafaidika vipi kutokana na dhana ya saizi zero?
4. Ni kina nani ambao wanazingatia sana dhana ya saizi zero?
5. Kulingana na utafiti ni yepi maoni ya watoto kuhusu miili yao?
6. Watoto wanajaribu kufanya nini ili wapate saizi zero?
7. Taja vyombo viwili vinazoelekezewa kidole cha lawama kwa habari juu ya saizi zero?

8. Ni maoni gani yanayowapotosha watoto katika magazeti?
9. Mwandishi anasihi wasichana wapewe suluhu gani tatu kuhusu swala la saizi zero?
10. Vyombo vya habari vinapewa mawaidha gani juu ya saizi zero?

**KIFUNGU C**

## MADHARA YA SEKTA ZA NGUO



Mahali kwingi kunako shughulika na utengenezaji wa nguo, si salama.Wanaofanya kazi katika viwanda vya nguo wanapaswa kuhamasishwa ili kutumia teknolojia safi ili kuzalisha bidhaa za kirafiki.

Sekta ya nguo hushirikisha matumizi ya nyuzi za asili kama vile pamba, hariri, katani, kamba, na vitu vinavyotengenezwa na wanadamu ambavyo kawaida ni nyuzi za sasini .Vitu hivi vyote huundwa kwakemikali ili viweze kufikia kiwango cha kuitwa nguo. Vitu hivi ni hatari kwanza kwa wanaofanya kazi

katika sekta hizi.Kwa wakati mwingi wafanyakazi katika sekta hizi wanaishia kupatwa na magonjwa yasiyo na tiba.

Viwanda vingine huwa havina vifaa vya kinga sahihi na hivyo huhatarisha usalama wa wafanyikazi. Hatari za afya katika sekta ya nguo ni pamoja na matatizo ya kurundikana pamoja, vumbi kutoka vipande vya kitambaa na, kwa upande wa rangi fulani ambayo husababishwa na kemikali yenye sumu.Ni jambo la hekima kuwa na vifaa vya huduma ya kwanza katika kila sekta ya kutengeneza nguo.

Utengenezaji wa nguo unasababisha uchafuzi wa mazingira kwa njia mbalimbali. Mabaki ya vitambaa vinavyokatwakatwa na kutupwa ovyoovyo huathiri mazingira. Mifugo wanaotangatanga wakila chochote, hawakosi kutafunatafuna mabaki haya ya nguo. Hii ni hatari kwa mifugo wenyewe na pia walaji wa nyama za mifugo ambao si wengine ila ni binadamu.Ikumbukwe pia kwamba kutapakaa kila mahali kwa mabaki haya huzuia mchanga lupumua hewa mchanga. Nguo zingine hutengenezwa kwavitambaa vya nailoni. Nguo za nailoni huchukua miaka 30 hadi 40 kuharibika. Hii husababisha mazingira kuchafuka. Ikiwa mabaki ya nguo za nailoni yanatupwatupwa katika mazingira, yanazuia kukua kwa mimea.

Katika sekta za nguo, vitambaa hupigwa rangi, huwekwa chapa kwa kutumia mashine.Baadhi ya mashine hizi hufusha moshi ambao unadhoofisha ubora wa hewa. Pia uchapishaji wa maandishi kwenye viwanda hivi vya nguo hutumia kiasi kikubwa cha maji na kemikali na kuchafua anga; jambo ambalo ni hatari sana kwa afya yetu.

Kwa mujibu wa Shirika la Kazi la Kimataifa, katika sekta ya nguo, watoto wanaajiriwa kama wafanyikazi. Jambo hili huwafanya watoto wengi kukimbilia ajira hii wakita kupata pesa kwa haraka.Ikumbukwe pia kuwa malipo wanayolipwa ni haba sana.Kwa wakati mwingi wanapewa kazi nyingi za kukata pamba, kushona kwa mikono, kushonea vifungo na kadhalika. Huu niunyanyasaji wa haki za watoto.Ajira kwa mtoto asiyefikisha umri ni hatia.

Kwa wakati mwingi wanaofanya kazi katika viwanda hivi vya nguo wananyanyaswa sana na waajiri wao.Wao hufanya kazi nzito sana lakini malipo ni

duni.Pia wanafanya kazi kwa saa nyingi sana ilhali wengi wao hulipwa kwa kibarua cha saa tu na wengine huishia kukaa kwa miezi bila malipo.Dhuluma kama hizi zinawafanya wafanyikazi wa sekta hizi kuishi maisha duni.



Wanaofanya kazi katika viwanda vya nguo wanakabiliwa na hatari nyingi kwa kiwango kikubwa.Ni jambo la kusikitisha kuona kwamba wengi hawana kinga ya maisha yao kwa vyovyote.Mwaajiri anapaswa kuwa na bima ya kuwakinga waajiriwa wake punde patokeapo mkasa wowote.Inaogofya kwamba maana wengi wa waajiriwa hawa ni vibarua wanaofanya kazi kwa masaa,siku au muda fulani, basi waajiri hawashughuliki na maslahi yao.Wengi wanaishia kupoteza viungo vya mwili kutokana na ajali za mashine,wasifidiwe na yeyote maana hawama bima.

Mahusiano ya waajiri na wajiriwa katika sekta hizi hayavutii hata kidogo.Waajiriwa wanachukuliwa kama mashine za kufanya kazi.Waajiri hawatambui haki za waajiriwa wao;kwa mfano, wengi hawaandikiani mkataba wowote baina ya mwajiri na mwajiriwa.Hii inaleta utata wa kutoaminiana kwa sababu kila upande unahisi kutoridhika na mwingine.Makubaliano ya kimaandishi ni muhimu sana katika kazi yoyote.

## MASWALI

1. Onyo la mwandishi kuhusu viwanda ni ipi katika aya ya kwanza?
2. Orodhesha vifaa vyenye kemikali ambavyo vinatumika viwandani.
3. Ni madhara gani ya kutumia vifaa hivi vyenye kemikali?
4. Taja hatari za kiafya zinazomkumba mfanyakazi wa viwanda vya nguo.
5. Taja viumbe vinavyoathirika kwa kutupwatupwa kwa vitambaa vya nguo?
6. Mchanga unaathiriwa vipi na viwanda vya nguo?
7. Eleza hasara za kutumia vitambaa vya niloni.
8. Watoto wanadhulumiwa kwa kuajiriwa katika viwanda vya nguo.Thibitisha kulingana na kifungu.
9. Toa sababu ya waajiri kutowachukulia wafanyikazi wao bima.
10. Waajiri hawajali maslahi ya waajiriwa.Thibitisha kulingana na aya ya mwisho.

**Kifungu D**

### UMUHIMU WA MAONYESHO KATIKA SEKTA YA NGUO

Maonyesho ya mitindo ya mavazi huwa na jukumu kubwa katika masoko ya nguo zinazozalishwa na sekta ya nguo. Hii huwa ni njia moja ya Utangazaji wa mtindo wa mavazi mbalimbali.

Maonyesho haya huchukua muda mrefu sana kutayarishwa na huitaji utaalamu na ujuzi wa aina yake.Hii husaidia kuyapa maonyesho yenyewe ladha ya kupendeza kwa mtazamaji.Maonyesho haya hunuiwa kuingiza mwelekeo wa mitindo ya hivi karibuni ili kumhamasisha mtazamaji .

Maonyesho haya ya mitindo huwa ni mbinu ya kuwasilisha kwa watazamaji bidhaa ili ziuzwe katika masoko.Wakati mtazamaji anaona mitindo hii,anaweza kuamua kununua nguo ya aina fulani na hii ni njia ya kuinua uchumi wa yule ameitengeneza.

Mitindo ya nguo hubadilika kila uchao.Maonyesho haya hufanyika mara kwa mara ili kuelezea na kuwasiliana na watazamaji kuhusu mwenendo wa hivi karibuni wa mitindo. Mwelekeo wa mitindo huendelea kubadilika mara kwa mara.

Utunzaji wa mtindo ni muhimu ili kutoa fursa ya mwenendo na mitindo tofauti ya nguo.Inawezekana kuwajulisha watu kuhusu hali ya sasa ya kubadilisha mitindo ya mavazi. Waumbaji wa mitindo huunda mifano mipya inayovutia wateja ili waweze kununua bidhaa.



Maonyesho ya mitindo ya mavazi hujenga jukwaa la kutambua ubunifuwa wanaoshiriki. Wengi hutambua, kwa njia ya maonyesho haya, ubunifu na vipaji vyao katika kubuni aina tofauti za nguo.

Kwa kushiriki katika maonyesho haya, wauzaji wanaweza kupata mitazamo mbalimbali ya nguo tofauti maridadi. Kwa kuangalia mtu akiigiza mtindo fulani wa mavazi, mtengenezaji anaweza kupata ujuzi juu ya aina tofauti za miundo na mitindo ya nguo ili iweze kuingizwa kwenye maduka ya kibinafsi.

Picha na video za mtindo zinazoonyeshwa husaidia wazalishaji wa viwanda vya nguo kuzalisha nguo za bei nafuu.

Watu wengi huchukulia maonyesho ya nguo kama njia ya kujigamba kwa wale wanaoshiriki maonyesho hayo.Mawazo kama haya ni potovu kwani watu wengi hunufaika kutokana na maonyesho haya.Jambo la muhimu ni kukumbusha wanaoshiriki kuonyesha mitindo ya nguo kwamba mavazi yanapaswa kuwa ya staha.Hivi majuzi kumetokea mitindo ya mavazi yanayomwacha mvaliaji nusu uchi.Kwa kweli nguo kama hizi hazina ladha yoyote katika wengi.Heshima idumishwe kwa maonyesho ya mitindo ya nguo.

**MASWALI**

1. Kulingana na aya ya kwanza, maonyesho ya nguo yana umuhimu?
2. Taja mambo mawili yanayosaidia kupendeza kwa maonyeshoya nguo.
3. Mtazamaji anafaidikajena maonyesho ya nguo kulingana na aya ya tatu?
4. Mtazamaji anapata mitindo mipya kutokana na maonyesho ya nguo.Toa sababu kulingana na aya ya tano.
5. Kulingana na kifungu, wanaoshiriki maonyesho haya wanafaidika vyovyote?
6. Wauzaji wanafaidi maonyesho ya nguo.Thibitisha.
7. Taja faida anazopata mtengenezaji kutoka kwa maonyesho ya nguo.
8. Bei nafuu ya nguo inatokea wapi kulingana na kifungu?
9. Sio kila mtu anachukulia maonyesho haya kwa njia chanya. Eleza kulingana na kifungu.
10. Mwandishi anawatahadharisha waigizaji wa mitindo ya nguo juu ya nini?

## Mada Ndogo ya 3: Sarufi

**Ukanushaji wa hali**

**Hali timilifu (me)**

Viambishi –ja-, -ha-, na –hu- hutumika kanusha vitenzi katika hali timilifu.
**Soma mifano ifuatayo**.

| Yakinishi | | | Kanushi | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Nafsi | Umoja | Wingi | Nafsi | Umoja | Wingi |
| Kwanza | Nimeandika | Tumeandika | Kwanza | Sijaandika | Hatujaandika |
| Pili | Umeandika | Mmeandika | Pili | Hujaandika | Hamjaandika |
| Tatu | Ameandika | Wameandika | Tatu | Hajaandika | Hawajaandika |

***Mifano zaidi:***

1. Tumeandika insha.
   Hatujaandika insha.
2. Wamewasili leo asubuhi.
   Hawajawasili leo asubuhi.
3. Amefunga shule.
   Hajafunga shule.
4. Nimemaliza kazi yangu ya ziada.
   Sijamaliza kazi yangu ya ziada.

**Zoezi**

**Kanusha sentensi hizi.**

1. Pahali hapa pamenipendeza.
2. Mvua imeshesha.

3. Sisi tumekimbia sana.
4. Mama amefua nguo.
5. Mwimbaji ameimba vizuri.
6. Kiti kimevunjika mguu.
7. Mti umekatwa na mkulima.
8. Jambazi limeshikwa.
9. Wanafunzi wamefunga shule.
10. Mtazamaji amefaidika na maonyesho ya nguo.

## Hali ya mazoea (hu)

Viambishi –hu-, -si-, -i-, -hu- na –ha- hutumika kukanusha vitenzi katika hali ya mazoea.

**Soma mifano ifutatyo.**

| **Yakinishi** | | | **Kanushi** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Nafsi | Umoja | Wingi | Nafsi | Umoja | Wingi |
| Kwanza | Mimi huchora. | Sisi huchora | Kwanza | Mimi sichori | Sisi hatuchori |
| Pili | Wewe huchora | Nyinyi huchora | Pili | Wewe huchori | Nyinyi hamchori |
| Tatu | Yeye huchora | Wao huchora | Tatu | Yeye hachori | Wao hawachori |

***Mifano zaidi***

1. Mimi hupenda michezo.
   Mimi sipendi michezo.
2. Wewe hula chakula kingi.
   Wewe huli chakula kingi.
3. Wavuvi huvua samaki wngi.
   Wavuvi hawavui samaki wengi.

## Zoezi

**Kanusha sentesni hizi.**

1. Daktari huwatibu wagonjwa wengi.
2. Baba hupenda kusoma gazeti.

3. Wavulana shuleni hucheza kandanda.
4. Mwalimu huchelewa darasani.
5. Mavazi ya Kiafrika huvutua.
6. Sisi hulima shambani.
7. Askari hushika doria.
8. Yeye hutembea vizuri.
9. Darasa lao hunuka.
10. Sara hunidanganya.

## Mada Ndogo ya 4: Kuandika

**Andika insha juu ya umuhimu wa mavazi ya Kiafrika.**

1. Taja mtindo wa mavazi ya kikwenu na ueleze kinachokuvutia katika mtindo huu.
2. Mavazi ya siku hizi hayaridhishi hata kidogo. Jadili.
3. Kazi katika viwanda vya nguo sio ya kuvutia.Toa maoni yako.

SURA YA
4

# HUDUMA ZA DHARURA

Mada
Ndogo 1:

Kusikiliza na kuzungumza

## Huduma ya kwanza:




Huduma ya kwanza inamaanisha huduma au msaada unatolewa kwa mtu anayekabiliwa na ugonjwa au madhara ya ghafla wakati daktarihayupo karibunakablahajapelekwahospitalinikwa matibabu zaidi.Kwa wakati mwingi wahudumu wa huduma ya kwanza waliohitimu huwa na kijisanduku chenye vifaa muhimu vya kuhudumia majeruhi wa ghafla.Mfano wa kijisanduku hicho ni kama huu:





Msalaba kwenye kisanduku cha huduma ya kwanzakati kati ya rangi ya kijani kibichi ni alama ya huduma ya kwanza. Ndani ya kijisanduku hiki huwana bendeji,dawa za majeraha zinazowekwa katika magari ilikutumika wakatiwa ajali.

Huduma ya kwanza inatolewa wakati mtu amejeruhiwa kwa shabaha ya kutunza uhai wake hadi daktari atakapopatikana au majeruhi atakapoweza kufikishwa hospitalini.Majeruhi wanaweza kuwa wanatokwa na damu. Sababu ya kutokwa na damu inaweza kutokana na pigo kubwa na kitu butu.Katika hali kama hii, kiasi cha kutokwa na damu inategemea kina na upana wa jeraha. Katika kisa hicho, unahitaji kutumia kipande cha nguo safi, kufunge jeraha. Baadhi ya sehemu nyingine za mwili kama kichwa zikijeruhiwa, itakuwa busara kuosha jerahakwa dawa kama iodini ili kuua bakteria. Ikumbukwe kuwa kitambaa kinachotumika kwa jeraha kinapaswa kuwa safi sana ili kumkinga majeruhi kutokana na kuambikizwa magonjwa mengine.

Shabaha nyingine ya huduma ya kwanza ni kuzuia kuongezeka kwa madhara kwa kumwondoa majeruhi kutoka kwenyasehemu yenye hatari kama moto, hatari ya mlipuko au mahali penye hatari.



Wakati unahudumia majeruhi, kuna mambo kadhaa unayopaswa kujua.Chukulia kwa mfano kisa kifuatacho.

Ukiwa safarini katika kijiji chenye watu wengi, unashuhudia ajali mbele yako. Inaonekana kwamba mtu aliyekuwa akivuka barabara pamoja na mkewe na binti yake mdogo aligongwa na gari.Mtu huyu amelala chini akivuja damu na hasongi.Mke na binti yake wako karibu naye.Mke wake analia na kutetemeka huku binti yake akisimama wima na kimya.Wanakijiji wachache wanakusanyika barabarani karibu na eneo la ajali.



Unahitaji kuchukua hatua ya haraka katika hali hii, lakini chukua wakati utulie kwanza naunapojiandaa kutoa usaidizi zingatia kama kuna mambo yoyote yanayokuhatarisha wewe au wengine,na jinsi utakavyoitatua hali hii. Ni jambo gani linalohitajika kufanywa kwa dharura hasa kwa mwanaume aliyejeruhiwa vibaya?

Unapofanya ukaguzi wa haraka wa ajali ile, unachunguza kama unaweza kukaribia eneo la ajali bila kujihatarisha kwani barabara hii ina magari mengi na bado kuna magari yanayopita karibu na waathiriwa na watazamaji. Pia unakisia kwamba yule mwanaume huenda aliumia vibaya.Ibua mazungumzo na walio karibu kwa mfano walioshuhudia ajali hiyo au wale wamefika kuokoa majeruhi.

## Maswali

1. Huduma ya kwanza ni nini?
2. Je, huduma ya kwanza inatolewa kwa majeruhi wa ajali pekee?
3. Ni nini umuhimu wa kisanduku cha Huduma ya Kwanza?
4. Kijisanduku cha huduma ya kwanza huwa na vifaa vipi?
5. Taja sababu tatu za kumpa mtu huduma ya kwanza.
6. Eleza sababu zinazoweza kufanya majeruhi avuje damu.
7. Ni nini upaswa kuangalia kwa mtu anayevuja damu?
8. Taja kifaa utakachotumia kuzuia kuvuja damu sana.
9. Kifaa hiki kinapaswa kuwaje na kwa nini?
10. Ni huduma ipi utampa majeruhi wa kichwa?
11. Taja sehemu mbili ambazo unaweza kumwokoa mtu kutokana na hatari.
12. Katika kisa cha ajali kilichonukuliwa hapa waliohusika kwenye ajali ni wangapi?
13. Taja mambo matatu unayopaswa kufanya kabla ya kuhudumia aliyejeruhiwa.
14. Ni jambo lipi unalopaswa kuzingatia juu ya barabara unapomhudumia majeruhi?

## Kifungu b:



Tukio linaloonekana kuwa dogo, linaweza kubadilika na kuwa kubwa. Aina za matukio ambayo yanaonekana kuwa madogo yanaweza kusababisha maafa, uharibifu mkubwa, kupoteza mali, au athari kubwa kwa mazingira.

Katika matukio kama haya huduma ya kwanza inahitajika sana. Kuna hatua ambazo unaweza kuchukua ili kukusaidia kabla, wakati, na baada ya tukio ili kupunguza athari zake bila kujali aina gani ya msiba au tukio ambalo linaweza kukuathiri wewe na familia yako. Ni jambo la hekima kutahadhari kabla ya tukio kutendeka kwa kusikiliza redio yako, televisheni, au taarifa na habari za dharura kutoka kwa viongozi wa umma.

Kuna hali zinazoitwa dharura ya matibabu. Dharura ya matibabu inaelezewa kama kuumia kwa papo hapo au hali ya matibabu ambayo inahitaji huduma ya haraka. Hali hizi zinaweza kuwa hatari kwa mgonjwa wa muda mrefu wa afya. Wakati unapopatwa na dharura ya matibabu, unahitaji kwanza kutambua iwapo ni dharura kubwa, ambayo inaweza kuwa hatari kwa maisha, au dharura madogo, ambayo sio.

Dharura kubwa ni hali ya uwezekano wa kutishia maisha ambayo inahitaji huduma ya haraka. Mgonjwa anayeonyesha dalili hizi yoyote inapaswa kupelekwa kwenye chumba cha dharura haraka iwezekanavyo, ili kuhakikisha matibabu sahihi yanatolewa kwa wakati unaofaa. Dharura kubwa za matibabu ni kama;Kupoteza fahamu, ishara za mushtuko wa moyo, ikiwa ni pamoja na maumivu kali ya kifua au shinikizo,ishara za kiharusi, ugumu kuzungumza, au kupoteza maono, kuumia kwa shingo au mgongo,mshtuko mkali au mshtuko wa

umeme,uwepo wa damu katika kukohoa au kutapika,mfupa ambao umevunjika kupitia ngozi.

Dharura ndogo ni hali ya matibabu ambayo haiishi hatari, lakini bado inahitaji huduma za matibabu ndani ya masaa ishirini na nne. Aina hizi za hali zinaweza kuhudumiwa kwenye kliniki za huduma za haraka.

Kuna aina mbalilmbali za matukio ya kufadhaisha kama vita, majanga ya kimaumbile, ajali, moto na vurugu baina ya watu kama vile dhuluma ya kimapenzi ambazo zinazotokea katika ulimwengu kila uchao. Watu binafsi, familia au jamii yote inaweza kuathiriwa. Watu wanaweza kupoteza maboma yao au wapendwa wao, wanaweza pia kutenganishwa na familia au jamii zao, au wanaweza kushuhudia vita, uharibifu au vifo.

Ingawaje kila mtu huathiriwa na matukio haya kwa njia moja au nyingine, kila mtu anaweza kuwa na hisia tofautitofauti. Watu wengi wanaweza kuhisi kulemewa, kuchanganyikiwa au wasiweze kujua kinachofanyika. Wanaweza kuhisi woga au wasiwasi au ganzi na kujitenga.Baadhi ya watu wanaweza kuwa na dalili dogo ilhali wengine wanaweza kuwa na dalili kali.Dalili za mtu hutegemea maswala mengi yakiwemo: hali na ukali wa matukio wanayopitia;ujuzi au tajriba yao ya matukio ya kufadhaisha yaliyopita; usaidizi walionao maishani mwao kutoka kwa wengine; afya yao ya kimwili; historia yao na ya familia yao kuhusu afya na matatizo ya kiakili; mila na tamaduni zao; nyakati kama hizi waathiriwa huhitaji huduma ya kwanza. Huduma ya kwanza ya usaidizi katika hali kama hizi ni msaada utolewao kutokana na utu ili kuwasaidia waliyo kwenye matatizo hayo. Huduma hii ya kwanza kwa wakati huu inahusu;Utoaji wa utunzaji halisi na usaidizi; Uchunguzi wa mahitaji na matatizo;Kusaidia watu kushughulikia mahitaji ya kimsingi,kwa mfano, chakula na maji;Kuwasikiliza watu bila kuwalazimisha kuzungumza, kuwasaidia kutulia;Kuwasaidia watu kupata habari, huduma na usaidizi wa kijamii; Kuwalinda watu dhidi ya madhara.

Kila mtu ana nguvu na uwezo wake wa kuwasaidia waathiriwa hawa kukabiliana na changamoto za maisha. Hata hivyo, baadhi ya watu hulemewa na huhitaji usaidizi zaidi katika hali ya dharura. Watu hawa wanaweza kujumuisha wale walio hatarini au wanaohitaji usaidizi zaidi kwa ajili ya umri wao kwa mfano watoto na wazee, wenye matatizo ya kiakili, au kikundi kilichotengwa au kilicholengwa na mkasa.

Kunaweza kuwa na hali ambapo mtu anahitaji usaidizi zaidi. Kwa mfano katika hali ya vita, unaweza kushuhudia hali mbalimbali za waathiriwa.Chukua kwa mfano wakimbizi wanaletwa kwa lori katika makao mapya na kufahamishwa kwamba watakuwa wakiishi humo.Walihamishwa kufuatia vita katika makao yao.Wanaposaidiwa kushuka kutoka kwenye lori, baadhi yao wanalia, wengine wanaonekana kushtuka, wengine wamechanganyikiwa huku wengine wakionekana kufarijika. Wengi wao wameshtuka na kuyashuku makao haya mapya, na hawajui watakapolala, kula wala kupokea matibabu. Wengine wanaonekana kushtuka wanaposikia sauti kubwa, wakifiri ni milio zaidi ya bunduki. Umejitolea kuhudumu kupitia shirika linalotoa vyakula, hivyo umeombwa kusaidia katika vituo vya kugawia chakula.

## Zoezi

1. Taja matokeo ya matukio yanayoonekana kuwa madogo.
2. Taja mbinu ya kutahadhari kabla ya tukio la mkasa.
3. Dharura ya matibabu ni nini?
4. Kuna aina ngapi za dharura za matibabu?
5. Orodhesha aina za dharura kubwa.
6. Dharura ndogo ni zipi?
7. Orodhesha matukio ya kufadhaisha yanayotukia katika ulimwengu wa leo.
8. Taja matokeo ya matukio ya kufadhaisha.
9. Kulingana na kifungu, orodhesha dalili tano zinazompata mwathiriwa wa mikasa.
10. Dalili hizi hutegemea nini?
11. Huduma ya kwanza utakayowapa waathiriwa hawa ni ipi?

12. Taja makundi matatu ya watu yanayohitaji usaidizi wa dharura zaidi kuliko wengine kunapotokea mkasa.
13. Kulingana na kifungu waathiriwa waliohamishwa na kupelekwa kwingine walikuwa na hali tofauti. Zitaje hali hizi.
14. Katika mazungumzo ya kuigiza kwa nini msimulizi anachagua kuongea na mtoto?
15. Eleza jinsi mazungumzo haya yanadhihirisha huduma ya dharura.

**Kwa makundi mawili, mawili, igigeni mazungumzo yafuatayo**

Zua mazungumzo na mtoto asiyeandamana na jamaa zake Kama vile:

| | |
|---|---|
| Wewe: | *[Ukipiga goti hadi kufikia kimo cha macho yake].*Jambo, jina langu ni__________.Nafanya kazi na shirika la _______________ na niko hapa kukusaidia.Jina lako nani? |
| Mtoto: | *[Huku akitazama chini na kuzungumza kwa sauti ndogo]*. Ni Musa. |
| Wewe: | Jambo Musa. Umekuwa na safari ndefu sana kuja hapa.Unahisi kiu?[Mpe chakula au kinywaji, msaada wowote kama vile blanketi ukiwa unao.] Familia yako iko wapi? |
| Mtoto: | Sijui *[akianza kulia]*. |
| Wewe: | Najua unaogopa, Musa. Nitajaribu kukusaidia kukuunganisha na watu watakaokusaidia kutafuta familia yako. Utaniambia jina la familia yako na nyumbani kwenu ni wapi? |
| Mtoto: | Ndio, mimi ni Musa Mangi. Natoka kijiji cha _______________. |
| Wewe: | Asante, Musa. Familia yako uliiona mwisho lini? |
| Mtoto: | Dada yangu mkubwa alikuwepo lori zilipokuja kutuleta hapa. Lakini sasa simwoni. |
| Wewe: | Dada yako ana miaka mingapi? Jina lake ni nani? |
| Mtoto: | Anaitwa Rose. Ana umri wa miaka 15. |
| Wewe: | Nitajaribu kukusaidia kumtafuta.Wazazi wako wako wapi? |
| Mtoto: | Sote tulitoroka kutoka kijijini tuliposikia milio ya risasi. Tulipotea kutoka kwa wazazi wetu. *[akilia]* |
| Wewe: | Pole sana, Musa.Najua uliogopa sana, lakini sasa uko salama. |
| Mtoto: | Naogopa! |
| Wewe | [kwa njia ya kirafiki]: Naelewa.Ningetaka kukusaidia. |

| | |
|---|---|
| Mtoto: | Nifanye nini? |
| Wewe: | Naweza kukaa nawe kidogo, na sote tujaribu kumtafuta dada yako.Ni sawa? |
| Mtoto: | Ndio, asante. |
| Wewe: | Kuna jambo lingine lolote linalokusumbua au kitu unachohitaji? |
| Mtoto: | Hapana. |
| Wewe: | Musa, inafaa tuzungumze na watu wale ili watusaidie kumtafuta dada yako au watu wengine wa familia.Tutaenda pamoja kuzungumza nao. *[Ni muhimu kumsaidia mtoto yule kujisajili na shirika linaloaminika la kutafuta familia au kuwalinda watoto kamalikiwepo.]* |

Mazungumzo kama haya ni huduma ya kwanza kwa sababu yanasaidia kujua chanzo cha mkasa na jinsi ya kusaidia mtoto asiye na fahamu kuhusu waliopo jamaa wake.

## Mada Ndogo ya 2: Sarufi

### Alama za Uakifishaji

Kunazo alama nyingi zinzotumika kuakifisha maneno na sentnsi katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya alama hizi ni kama vile:

#### a) Herufi kubwa

*Matumizi*

1. Kuanzisha sentensi.
2. Kuonyesha nomino za pekee. Kwa mfano, Bi Manzu anaishi Juba.

3. Kuonyesha kichwa au mada.
4. Kuonyesha maneno yaliyofupishwa.

### b) Alama ya kituo kikuu/kikomo (.)

*Matumizi*

1. Kuonyesha mwisho wa sentensi.
2. Katika kufupisha maneno.
3. Kuonyesha saa.
4. Katika hesabu kuonyesha sehemu isiyo nzima.
5. Kuonyesha senti katika pesa.

### c) Alama ya koma (,)

*Matumizi*

1. Kuorodhesha vitu zaidi ya mbili.
2. Kugawanya mawazo katika sentensi.
3. Kutoa maelezo zaidi.
4. Katika tarakimu, kugawa elfu.

### d) Alama ya kiulizi (?)

*Matumizi*

1. Kuulizia swali.
2. Kuonyesha pengo lililoachwa wazi.

### e) Alama ya hisi (!)

*Matumizi*

1. Kuonyesha hisia kama vile hasira, mshangao, furaha n.k.
2. Kuigiza tanakali za sauti.

### f) Alama ya koloni/nukta mbili (:)

*Matumizi*

1. Kutanguliza orodha.
2. Kuonyesha sababu au matoke ya kitu.
3. Kuonyesha saa.
4. Kunukuu ukurasa kwa Bibilia.
5. Kuonyesha maneno ya msemaji katika mchezo wa kuigiza.

6. Kuonyesha mada katika barua au kumbukumbu za mkutano.

### g) Alama ya semi-koloni (;)

*Matumizi*

1. Kuorodhesha vitu vinapokuwa na Zaidi ya neno moja.
2. Kuonyesha mawazo mawili.

### h) Alama ya kistari kifupi (-)

*Matumzi*

1. Kuunganisha maneno mawili.
2. Kuonyesha hadi, au mpaka.
3. Kama alama ya kupunguza au kutoa katika hesabu.
4. Kuonyesha neno ambalo halijakamilika litaendelezwa katika mstari ufutao.
5. Kuonyesha tarehe.

### i) Alama ya kistai kirefu ( - )

*Matumizi*

1. Kutoa maelezo zaidi.
2. Kuorodhesha hoja au vitu.

### j) Alama ya mabano/parandesi ()

*Matumizi*

1. Kutoa maelezo Zaidi.
2. Kutoa neno jingine lenye maana sawa.

### k) Alama ya kinyota (*)

*Matumizi*

1. Kuonyesha neno ambalo litelezewa zaidi chini ya ukurasa.
2. Kuficha herufi au silabi katika neno ili kungunguza ukali wa maneno yasiyo na nidhamu.

### l) Alama ya mlazo (/)

*Matumizi*

1. Kuonyesha ‘au’.
2. Kuonyesha neno au fungu la maneno lenye maana sawa.

3. Katika hesabu kuonyesha kugawanya au akisami.
4. Katika tarehe.

**m) Alama ya kunukuu (“ ”)**

*Matumizi*

1. Kunukuu usemi halisi.
2. Kunukuu kichwa cha kazi ya saa k.v kitabu, wimbo, kipindi n.k.
3. Kuonyesha maneno yasiyo ya Kiswahili unapochanganya ndimi katika sentensi.
4. Kuonyesha maneno yanayowakilisha maana tofauti na maana yake ya kawaida au kinaya.
5. Kuonyesha herufi iliyoanchwa nje au kufupisha maneno katika ushairi hasa kwa kusudi la kutosheleza idadi ya mizani.
6. Katika maendelezo ya sauti ya ung’ong’o (ng’).

## Zoezi

**Akifisha kifungu hiki.**

kwa upande wa utunzaji wa utamaduni mitindo ya kiafrika ya mavazi inavutia si haba mitindo yake ina rangi mahiri za kupendeza na zenye sifa maarufu rangi kama hudhurungi samawatikijani na wakati mwingine mchanganyiko wa rangi mbalimbali unavutia macho mitindo ya mavazi ya kiafrika humulika mila na utamaduni wa kabila fulani hii hupelekea kuzipa mizizi mila na tamaduni za watu hawa umaarufu usioweza kuondolewa kwa haraka.

## Mada Ndogo ya 3: Kuandika

1. Umeshuhudia kisa cha vita.Eleza madhara yake.

2. Jirani yako amevamiwa na wezi.Elezea hatua za dharura utazofuata kumwokoa.
3. Mtoto wako amepaliwana chakula.Ni huduma zipi za kwanza utakazotumia kumwokoa.

# SURA YA 5

# TEKNOLOJIA

## Mada Ndogo ya 1: Kusikiliza na Kuzungumza

Vifaa vya kiteknolojia



**Kompyuta**



**Tarakilishi**



**Kikokotozi**



Rununu



Simu ya mezani



Kipaza sauti

Sekta ya mawasiliano ni mojawapo ya sekta muhimu katika maendeleo ya nchi yoyote ile. Bila ya kuwepo kwa mawasiliano mwafaka, uchumi wa nchi hulegalega na kudidimia. Tangu jadi binadamu waliwasiliana kwa njia anuwai.

Umuhimu wa sekta hii ya mawasiliano katika ulimwengu wa leo, hauwezi kamwe kupuuzwa. Bila kuwapo kwa mawasiliano bora, hasa katika sekta ya usafiri, bidhaa nyingi huweza kuozea maghalani na hata mashambani kwa sababu ya ukosefu wa magari ya kuzifikisha sokoni kuuzwa. Aidha, sehemu zisizo na barabara nzuri hubaki nyuma kimaendeleo. Hii ni kwa sababu wananchi wengi ambao wangejibiidisha kuinua sehemu hizo hawataki kuishi pahala pasipo na njia na mawasiliano bora.

Maendeleo yamefikiwa katika sekta hii ya mawasiliano. Huduma za simu zimeimarika si haba kwa sababu ya kuwapo kwa kampuni mbalimbali za kutoa huduma ya mawasiliano kama vile simu, ambazo hujulikana kama simu-tamba. Tangu kuvumbuliwa kwa simu hizi, wananchi wengi ambao hata hawangeota wala kufikiria kuwa na simu wameweza kujinunulia simu hizi. Mawasiliano yameimarika hata katika sehemu za mashambani kwani watu wengi huweza kuwasiliana na jamaa zao,walio mijini wakiwa mashambani.

Kampuni mbalimbali zimeweza kutoa ushindani mkubwa katika huduma hii ya usambazaji wa simu kwa wananchi. Mashindano haya yanahimiza zaidi wananchi kuwa na simu. Hili ni jambo la kutia moyo.

Uvumbuzi wa mitambo ya kompyuta umechangia pakubwa kukuza mawasiliano bora. Siku hizi ulimwengu umekuwa kama kaya moja kubwa. Kumekuwa na mtandao wa mawasiliano ya kimataifa wa kikompyuta. Kupitia kwa mtandao huu, nchi nyingi zimeweza kufaidika sana kimawazo kwani wataalamu na hata wasomi wengi wameweza kupata mawazo na maoni mbalimbali kuhusiana na masuala mengi yanaoathiri jamii zao.

Fauka ya hayo kuna ule ugunduzi wa barua pepe ambao umerahisisha mawasiliano na kuyafanya ya bei nafuu. Siku hizi mtu anaweza kuwasiliana na

sahibu yake akiwa mbali kwa gharama ya shilingi chache tu! Kompyuta nazo zimerahisisha kazi kwani huweza kuhifadhi jumbe tofauti na mashine za kijadi za upigaji chapa. Kwa wale wanaohitaji kutumia simu tamba mno, wanaweza kutuma ujumbe kwa simu hizo hizo kwa gharama nafuu badala ya kupiga simu.

Teknolojia imeibua mitandao ya kijamii ambayo ina faida chungu nzima. Kwa mfano, mitandao ya kijamii inawasaidia watu kutengeneza mahusiano mapya kati ya ndugu na marafiki na pia inaongeza mawasiliano kati ya mtu na mtu na hivyo kuboresha mahusiano.

Mitandao ya kijamii imesaidia kuwaleta watu pamoja wenye mitizamo inayofanana. Mitizamo ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni, kimapenzi, kimichezo na kadhalika. Watu ambao wamekuwa na matatizo ya kuongea siku hizi wanajisikia huru kuwasiliana na watu kupitia mitandao ya kijamii. Imekuwa niuwanja mzuri wa mtu kujionyesha kwa kile alicho nacho moyoni mwake na kukifikisha kwenye jamii.

Baadhi ya watumiaji wa mitandao hii ya kijamii wamekuwa wakiitumia kutafuta hata kazi, wanafunzi wamekuwa wakiitumia kufanya majadiliano ya kimasomo, wanaharakati wametumia majukwaa ya mitandao ya kijamii kukutana na kuendesha harakati zao. Vyuoni hususani wamekuwa wakiendesha harakati za ufunzaji kupitia mitandao ya kijamii.

Baadhi ya watu wameitumia mitandao ya kijamii kupunguza misongo ya mawazo kwa kuwasiliana na watu mbalimbali na kujikuta wamefarijika katika matatizo waliyonayo. Wataalamu wa saikolojia wanashauri mtu anapokuwa na matatizo ni vyema akaishirikisha jamii ili kupunguza mzigo wa kuchukua matatizo peke yake.

Mitandao ya kijamii kwa sasa imekuwa ikipanua wigo wake wa mawasiliano kutoka kuwa mitandao ya kijumla  na kuwa bayana zaidi. Kwa mfano watu wamekuwa wakitengeneza makundi ya fani fulani ambapo inawasaidia waliotengeneza fani hiyo kukutana pamoja mtandaoni na hata kuongeza wigo wa

kukutana uso kwa uso. Na hii imesaidia watu ambao wamekuwa wanataka kuingiza kwenye makundi ya fani hizo waweze kujumuika nao pamoja.

Ijapokuwa teknolojia imesaidia maendeleo ulimwenguni,kwa upande ule mwingine imeleta madhara mengi si haba. Kwa mfano,watu wanatumia wakati wao mwingi sana katika mazungumzo na kuangalia picha kwenye simu tamba.Wengi wao wanatumia hela si kidogo kwa kuwasiliana na wengine.

Katika vyombo hivi vya teknolojia, utovuwanidhamu umetokea. Kwa mfano vijana wameingia katika mawasiliano yasiyofaa na wengine. Hii imesababishwa utapeli, wizina udanganyifu wa kila aina.Kutokana na hali kama hizi, vijana wengi wamejipata kwenye matatizo wasiyoyakusudia na wasioweza kujinasua.Picha chafu za kimapenzi zimetawala vyombo vya teknolojia zikiwemo simu tamba, tarakilishi, videona kadhalika.Vijana wengi hupoteza wakati wao mwingi sana wakiziangalia picha hizi zenye mafunzo hasi.

Mitandao ya kijamii nayo imewafanya watu kutumia muda mwingi kuwasiliana mitandaoni na kuwafanya kuwa wazembe sana kuwasiliana uso kwa uso.

Vijana wengi wanaoibukia kwa sasa hasa wenye umri kuanzia miaka kumi na mitatu wako kwenye wakati mgumu sana kuathirika na matumizi ya mitandao ya kijamii. Vijana wengi wanaenda wakieleza habari zao kwenye mitandao hii ya kijamii,hawajui kwamba taarifa mbalimbali wanazoziweka mitandaoni ni taarifa ambazo zinaonekana kila mahali hata kama zikifutwa taarifa hizo zinaweza zikapatikana tu.

Vijana wengi wameingia kwenye mitego kwa uelezaji mwingi wa taarifa za mtu binafsi. Habari hizi zinaweza kumfanya mtu kuwa muhanga wa mapenzi au kuingizwa katika wizi wa fedha na ujagili mitandaoni. Watu wanatumia taarifa hizo kufanya uhalifu. Kwa hivyo vijana wanatakiwa kuwa makini na taarifa zao wanazoziweka mitandaoni. Hii inaweza kusababisha hata mtu kufukuzwa kazi kama mtu anaweza kutoa taarifa fulani za mwajiri ambazo zinaweza kuleta mkanganyiko kwenye taasisi fulani.

Matumizi ya vyombo vya teknolojia yamezua migogoro katika familia. Muda wa kukutana uso kwa uso kwa ajili ya kubadilishana mawazo umepungua sana kwa sababu ya ongezeko la watu kutumia muda mwingi sana kwenye mitandao ya kijamii. Wazazi wamekuwa na muda mchache wa kubadilishana mawazo na watoto wao, nao watoto wamepata fursa ya kuangalia chochote wanachotaka kwenye mitandao.

Utafiti mmoja ulionyesha kwamba theluthi mbili ya wafanyakazi wanaotumia wakati mwingi wa kazi kubadilishana mawazo na watu mitandaoni wakati wa kazi. Kwa maneno mengine wafanyakazi hawa wanaiba muda wa mwajiri wao. Ofisi za serikali hakika wamekuwa na changamoto kubwa sana kwa wafanyakazi wao wanaotumia mitandao ya kijamii kwani utendaji wao kazi hakika umepungua kwa sababu watu wanatumia muda mwingi sana kwenye mitandao ya kijamii wakati wa kazi.

## MASWALI

1. Sekta ya mawasiliano ina manufaa gani kwa nchi?
2. Eleza hasara za kukosa mawasiliano katika sekta ya usafiri.
3. Taja upungufu wa kutokuwa na barabara nzuri.
4. Wananchi wamefaida vipi kutokana na uvumbuzi wa simu-tamba?
5. Je mashindano ya kampuni za huduma ya mawasiliano yana manufaa yoyote?
6. Eleza manufaa ya mtandao wa kimataifa.
7. Taja vile barua pepe imerahisisha mawasiliano.
8. Mahusiano ya watu imeboreka vipi kupitia kwa mitandao ya kijamii?
9. Ni mitazamo ipi ambayo imeimarika kutokana na mitandao ya kijamii?
10. Eleza faida za mitandao ya jamii kwa wafuatao:
    - i) wanafunzi
    - ii) wanaharakati
    - iii) Vyuo

11. Mitandao ya jamii imesaidia watu walio na shida nyingi za kufikiria.Thibitisha kutokana na kifungu.
12. Makundi yanayoundwa mitandaoni yamefaida vipi kutokana na mitandao?
13. Kulingana nakifungu, watu wanaharibu wakati kwa simu tamba kwa njia gani?
14. Je wanaonaswa sana na visa vibaya vya vyombo vya teknolojia ni kina nani? Thibitishakwa hoja mbili.
15. Wafanya kazi wengine hawajawajibika.Thibitisha kulingana na aya ya mwisho.

**Kifungu b:**

## Umuhimu wa teknolojia katika kufunza

Mikakati ya kufundisha kulingana na teknolojia ya elimu inaweza kuelezewa ufanisi mkubwa ambao unawezesha kujifunza kwa wanafunzi na kuongeza uwezo wao, uzalishaji, na utendaji.Ushirikiano wa teknolojia katika elimu husababisha mabadiliko mazuri katika mbinu za kufundisha.

Vifaa vya teknolojia vinafanya ufundishaji rahisi. Kama una uchovu wa kutoa maelezo ya kinadharia au wanafunzi wako hawawezi kuelewa na kile unachofunza, basi matumizi ya vifaa vya kiteknolojia vinasaidia sana katika hali kama hii.

Vifaa vya teknolojia katika ufunzaji ni njia ya kuwasilisha dhana ngumu ambayo inafanya dhana wazi kwa kila mwanafunzi katika darasa. Wanafunzi wako wataelewa hasa jinsi ujuzi hutumiwa katika mazoezi. Unaweza kutumia vidonge na maonyesho ya kompyuta ili kutoa aina yoyote ya somo au maelekezo na kuboresha kiwango cha ufahamu ndani ya darasa.

Teknolojia inakusaidia kufuatilia maendeleo ya wanafunzi wako.Kuhifadhiujumbe na alama za wanafunzi wako kwenye tarakilishi, ni njia mojawapo ya kujua na kufuatilia maendeleo ya wanafunzi wako.

Teknolojia ya elimu husaidia uhifadhi wa mazingira.Je, unaweza kufikiri kiasi cha karatasi na idadi ya miti ambayo ingeweza kuokolewa iwapo kila shule iliamua kuanzisha vitabu vya digitali? Bila shaka, lengo hilo ni mbali na kweli wakati huu, lakini unaweza kufanya mabadiliko kwa kuwafundisha wanafunzi wako kuchukua ujumbe kwa mtandao na kuwasilisha karatasi zao na kazi za nyumbani kupitia barua pepe.

Vifaa vya teknolojia vinampa mwanafunzi nafasi ya ujifunzaji.wanafunzi hufurahia kujifunza.Sio kila wakati mitandao inawazuia wanafunzi kutoka kwenye mchakato wa kujifunza, mwalimu anaweza kutumia mwelekeo wao wa kutumia muda mtandaoni kwa kusudi nzuri kwa kujifunza ili kujifurahisha.Tumia teknolojia ya skrini ya kugusa na maonyesho ya mtandaoni ili kufanya madarasa zaidi ya mwingiliano. Unaweza pia kutegemea teknolojia wakati unataka wanafunzi wako kushiriki katika majadiliano. Weka kikundi cha kibinafsi cha darasa lako kwenye simu na uhamasishe mazungumzo yenye kujenga.

Teknolojia hufanya kujifunza kwa kina kueleweka zaidi kuliko hapo awali.Bila maajabu ya mtandao, watu hawataweza kufikia aina yoyote ya habari wakati huu wanaofikiria. Leo, kujifunza kwa kina ni mojawapo ya mbinu za kujifunza zaidi zinazoendelea. Masomo ya kweli yanaendelea kuchukua nafasi ya mihadhara ya jadi. Wanafunzi wanaweza kuandaa wakati wao kwa njia ambayo huwafanyia kazi, na wanaweza kupata kwa urahisi maarifa wanayopenda. Kwa mfano, hebu sema mmoja wa wanafunzi wako anaonyesha ujuzi mkubwa katika funzo fulani, lakini mtaala wa jadi haufanyi kitu cha kuwapa ujuzi wa funzo hilo kwa vyovyote.Basi unaweza kuwaelekeza kwa mafunzo ya mtandaoni ambayo yanatoa mafunzo haya kwa hali ya juu.

Nafasi ya teknolojia katika kufunza ni kuwa wanafunzi na walimu wanaweza kupata habari wakati wowote.Hii ni uwezekano wa faida zaidi ya teknolojia. Zamani walimu wa shule walikuwa wanafunzi kwa vile walipaswa kutumia saa kadhaa kwenye maktaba ili kutafuta habari waliyohitaji. Leo, u teknolojia

hufanya kila kitu tofauti na rahisi. Wanafunzi wanaweza kupatakwa urahisi magazeti, makala za kisayansi, masomo, na aina nyingine yoyote ya maudhui mtandaoni. Wanaweza kuandika karatasi bora za kitaaluma za kina kwa sababu wanaweza kusaidia hoja zao na ushahidi zaidi.Unapotoa hotuba wanafunzi hawaelewi, wanaweza kupata maelekezo na habari rahisi na utafutaji mmoja *wa Google.*

Teknolojia inafanya ushirikiano ufanisi zaidi katika ufunzaji.Wakati mwingine ushirikiano katika mazingira ya darasa unakuwa nahitilafu, kwa mfano, unaandaa makundi, washiriki miradi, na ghafla darasa linakuwa fujo kamili. Wanafunzi wengine huelezea maoni yao kwa sauti kubwa na imara, wakati wengine hawapati nafasi ya kusikilizwa. Vifaa vya mtandaoni na programu hutoa mipangilio ya kipekee kwa wanafunzi kushiriki katika mradi wa kikundi. Wanaweza kufanya kazi kutoka nyumbani; timu inaunganishwa kwanjia ya mtandao na kila mtu anaongozwa na mazingira yaliyotulivu.Kwa hivyo Faida za kushirikisha teknolojia katika ufunzaji ni nyingi si haba,ni vyema mwalimu azishirikishe katika ufunzaji wake.

**MASWALI**

1. Kulingana na aya ya pili vifaa vya teknolojia vinasaidia katika hali gani ya ufunzaji?
2. Dhana ngumu darasani usuluhishwa vipina vifaa vya teknolojia?
3. Utawajuaje wanafunzi wako kupitia kwa teknolojia?
4. Teknolojia inawezaje kusaidia mazingira?
5. Taja umuhimu wa barua pepe katika utafiti wa mwanafunzi.
6. Fafanua mbinu ambayo mwalimu anaweza kutumia kwa mwingiliano wa wanafunzi.
7. Ujifunzaji hutamsaidia mwanafunzi vipi?
8. Mwandishi anamaanisha nini anaposema zamani walimu walikuwa wanafunzi?
9. Je programu za mtandaoni zinasaidiaje kulingana na kifungu?

## Mada Ndogo ya 2: Sarufi

### VIVUMISHI

Vivumishi ni maneno yanayotumika katika lugha ya Kiswahili kuelezea zaidi kuhusu nomino. Mara nyingi, vivumishi hutanguliwa na nomino.

## Aina za Vivumishi

#### a) Vivumishi vya sifa

Vivumishi hivi hutoa sifa kuhusu kitu, mtu, mahali n.k. Mifano ni kama vile safi, baya, kali, tamu.

1. Sauti nzuri humtoa nyoka pangoni.
2. Mama hupika chakula kitamu.

#### b) Vivumishi vimilikishi

Hivi vivumishi hutumika kuonyesha kuwa nomino inamiliki nyingine. Mizizi ya vivumishi hivi huundwa kulingana na nafsi mbalimbali (-angu, -ako, -ake, -etu, -enu, -ao).

Mifano:

1. Mwalimu aliweka kitabu chako kabatini.
2. Amepata shati lake katika pipa la uchafu.

#### c) Vivumishi vya idadi

Hivi hutuelezea Zaidi kuhusu kiasi, au idadi ya nomino. Kuna aina mbili.

i) Vivumishi vya idadi kamili

Vivumishi hivi hutumia nambari kuelezea idadi ya nomino.

1. Mwanafunzi mmoja amewatega ndege wawili.
2. Siku saba zimepita tangu mama kuvunjika mguu.

ii) Idadi isiyodhihirika

Vivumishi hivi huelezea kiasi cha nomino kwa ujumla, bila kutaja idadi kamili.

1. Walimu wachache walihudhuria mkutano.
2. Chakula kidogo kitawatosha.

### d) Vivumishi visisitizi

Hivi vivumishi husisitiza nomino fulani kwa kurudia rudia kivumishi kiashiria.

1. Ng’ombe yuyu huyu
2. Kalamu ii hii
3. Uteo ule ule

### e) Vivumishi viashiria/vionyeshi

Vivumishi hivi hutumika kuonyesha au kuashiria nomino kulingana na mahali.

| | |
|---|---|
| Karibu | hapa, huyu, hiki, hili, huku, haya, ule, wale, pale |
| Mbali kidogo | hapo, huyo, hiyo, hicho |
| Mbali zaidi | pale, lile, kile, ule |

1. Mvulana huyu ni mrefu kuliko yule.
2. Matunda haya yameiva.
3. Samaki hao wanavunda.

### f) Vivumishi viulizi

Hutumika kuuliza swali. Baadhi ya vivumishi viulizi huchukua viambishi vya ngeli.

1. Ni wanafunzi wangapi waliofika shuleni?
2. Ni mtu upi uliokatwa?
3. Ni gali lipi lililoshikwa na polisi?

**Kunavyo vivumishi viulizi vingine ambavyo havichukui viambishi vyovyote.**

1. Je, mmefika wapi?
2. Unazungumzia kuhusu shati gani?

### g) Vivumishi virejeshi

Vivumishi hivi hurejelea nomino. Vinaweza kuwa vivumishi vya O-rejeshi au vivumishi viashiria vinapotumika kurejelea nomino.

1. Daktari ambaye alikuja ni mrefu.
2. Kicheko cha kutisha ambacho ulisikia ni cha mgonjwa yule.

### h) Vivumishi vya KI-Mfanano

Hivi hutumika kulinganisha sifa ya nomino na hali au tabia nyingine.

1. Mwalimu mkuu hutembea kifalme.
2. Vijana siku hizi wanapendelea kusikiliza miziki ya kizungu.

### i) Vivumishi ya A-Unganifu

Hivi vivumishi hutuelezea Zaidi kuhusu nomino kwa kuonyesha kitu kinachomiliki nomino hiyo. Huundwa kwa kuambatanisha kiambishi cha nfsi/ngeli pamoja na kiambishi –a cha a-unganifu, kisha nomino.

1. Kiti cha mwalimu wetu ni kipya.
2. Gari la baba yangu litauzwa.

## Mada Ndogo ya 3: Kuandika

**Andika insha kuhusu faida za teknolojia.**


1. Simu tamba zimesababisha mengi kuliko manufaa. Jadili.
2. Eleza Umuhimu wa teknohama.


**Mada Ndogo ya 4:** Msamiati

## Dira ya dunia

Dira ya dunia hutumiwa kuonyesha pembe za dunia. Dira huwa na pembe nne kuu, nazo ni kaskazini, kusini, magharibi na mashariki.

**Wewe na wenzako, jadilianeni pembe nne za dira ya dunia.**






1. **KKM** - Kaskazini ya Kaskazini Mashariki

2**. KM** - Kaskazini Mashariki

3. **MKM** - Mashariki ya Kaskazini Mashariki

4. **MKM** -5. KM - Kusini Mashariki

6. **KKM**- Kusini mwa Kusini Mashariki

7**. KKM** - Kusini mwa Kusini Magharibi

8. **KM** - Kusini Magharibi

9. **MKM** - Magharibi ya Kusini Magharibi

10. **MKM** - Magharibi ya Kaskazini Magharibi

11. **KM** - Kaskazini Magharibi

12. **KKM** - Kaskazini mwa Kaskazini Magharibi

**Zoezi**

1. Pande mbili ambazo zimo baina ya kaskazini na mashariki ni zipi?

2. Jua huchomoza kutoka upande upi?

3. Jua hutua upande upi?

4. Ikiwa ni asubuhi, kivuli chako kitakuwa upande upi?

5. Ikiwa jua li kusini, kivuli chako kitakuwa upande upii?


6. Jua huwa upande upi wakati wa alasiri?

## Sayari

Sayari hupatikana angani, hulizunguka jua na hupata mwangaza kutoka kwa jua.
Binadamu huishi katika sayari moja ambayo ni dunia.
Sayari ambayo ni kubwa zaidi ni mushtarii au sumbla.

Sayari ambayo ni ndogo sana ni zebaki. Zuhura huitwa nyota ya alfajiri au nyota ya magharibi kwa sababu sayari hii hung'aa sana kabla ya jua kuchomoza.
Inaaminika mrihi inakaribiana kimaumbile na dunia.

Mkiwa kwa makundi ya wawili wawili, jadilianeni sayari z ilioonyeshwa kwenye picha ifuatayo.



## Zoezi

1. Sayari inayoweza kuonekana wakati wa mapambazuko ni ipi?
2. Ni sayari ipi iliyo mbali sana kutoka kwa jua?
3. Sayari ya tatu kutoka kwa jua ni ipi?
4. Sayari kubwa zaidi ya zote ni ipi?
5. Kuna sayari ngapi?

# SURA YA 6

# AJIRA

**Mada Ndogo ya 1:** Kusikiliza na kuzumgumza

Kifungu a

## NJIA ZA KUPATA AJIRA



Ajira huwa ni neno linalomaanisha kazi ya kudumu au kazi ilio na mshahara.

Kuna njia mbili za kupata ajira, kwanza mtu anaweza kuajiriwa au ajiajiri.Ikiwa mja hataki kuajiriwa na wengine basi anaweza kujiajiri. Kuna sababu mbalimbali kwa nini mtu atake kuajiri, badala ya kuajiriwa, mfano kipato kidogo anachopata katika kazi husika, hitaji la kutaka uhuru zaidi binafsi wa kufanya kazi, hitaji la kuweza kutoa ajira kwa wengine na sana kuweza kutumia vyema kipaji na uwezo wa kuzalisha ambao katika kazi ya sasa mtu hapati nafasi ya kufanya hivyo.

Kujiajiri ni jambo linalohitaji maandalizi ya muda mrefu na kuna mambo ya msingi kuyafahamu, haiwezekani tu, ukaacha kazi na kusema unajiajiri. Kuna mambo ya msingi ya kujiandaa na kuyafahamu kabla mtu hajaamua kuacha kuajiriwa,kama vile; kuwa na mkakati ni jambo muhimu: Wazo au ndoto isiyo na mkakati wa kuitimiza haina maana.Hivyo basi ndoto yako ya kujiajiri siku moja, ni lazima iwekewe mkakati wa kuifanikisha ikiwa ni pamoja na muda hasa wa lini utaitimiza hiyo ndoto.

Katika kuweka mkakati huu wa kutimiza ndoto yako, fanya utafiti wa kina kuhusu mipango yako binafsi ya maisha, mtazamo wako kuhusu maisha, mpenzi/mke wako, familia yako, na hali ya jamii kwa ujumla inavyoenda kama vile mabadiliko ya hali ya kisiasa, teknolojia, na uchumi.

Tengeneza malengo ya aina ya shughuli unayotaka kuifanya ukiacha kuajiriwa, na pima uwezekano wa shughuli hiyo kufanyika kweli na kama itakulipa. Utambue pia aina ya watu na rasilimali nyingine utakazozihitaji, na jinsi utakavyozipata.

Hitaji la fedha ni muhimu sana katika kujiajiri. Unahitaji kiasi cha fedha za kutosha kununua vifaa na malighafi ya kutengenezea bidhaa yako. Pia unahitaji fedha za kuwalipa wafanyakazi wako, na zaidi sana, unahitaji fedha za kuendesha maisha yako na familia yako, kwa kipindi fulani kabla ya biashara kuanza kukulipa mshahara. Hivyo kabla haujaacha kibarua chako, hakikisha umetengeneza bajeti ya kutosha na una akiba ya kutimiza mahitaji ya bajeti

yako. Usingependa uache kazi halafu uanze kuombaomba kwa rafiki na jamaa, au uanze kujuta.

Ni lazima ufahamiane na watu mbalimbali. Kumbuka katika kujiajiri kwako, utahitaji wateja, washirika, wafanyakazi na hata washauri mbalimbali ili mambo yako yaende vizuri. Hivyo, wakati ukiwa umeajiriwa ndio wakati wako muafaka wa kutengeneza na kupanua wigo wako wa watu unaowafahamu na waliokaribu nawe.

Kumbuka kuendeleza mawasiliano kwani watu hawapendi kuona wewe unataka kuwatumia tu kisha unawatupa. Endeleza mawasiliano walau hata kwa salamu tu. Zaidi sana, heshimu watu wote, hata usiowafahamu au wale unaodhani 'sio watu muhimu. Jenga taswira nzuri kwa jamii kwa lugha fasaha, picha na matukio mengine, usifanye watu wakufikirie vibaya.

Ikiwa unataka kujiajiri usipitwe na wakati. Hakikisha kuwa unafuatilia taarifa za matukio, jihusishe na watu wanaohusiana na aina ya shughuli unayopanga kuifanya wakati utakapojiajiri. Hii itakusaidia kupata uzoefu na kusoma ishara za nyakati, na pengine kutambua fursa nyingine zaidi.

Endelea kujifunza zaidi kuhusu kazi yako, watu na jamii kwa ujumla kwani kujiajiri kunahitaji uzoefu zaidi, na zaidi sana uwezo wa kupambana na changamoto nyingi ambazo nyingine haujawahi kukutana nazo kabisa.Taarifa za awali na kujua jinsi mambo yanavyoenda kwa ujumla katika jamii vitakufanya ushinde changamoto.

Ni lazima uelewe maana halisi ya kujiajiri. Baada ya kuacha kuajiriwa, hautarajii kuwa mtu wa ‘kuganga njaa’ yaani kufanya biashara ili mradi tu hela iingie, lakini haujui mwelekeo wa biashara yako ukaje, na wala hakuna mkakati wa kuikuza na kuimarisha biashara husika.

Biashara inahusu kutimiza mahitaji ya watu, kwa hiyo ilimradi utakuwa na uwezo mkubwa wa kutimiza mahitaji ya watu, na kuendelea kuhamasisha watu zaidi kuja kwako uweze kutimiza mahitaji yao, basi biashara itakua, na itaendelea kuwa endelevu.

Kinyume cha hapo, ushindani utakuondoa katika biashara kwani wateja watakimbilia kwa wengine. Biashara sio tu kupata wateja, ni vile unaweza kuendelea kupata wateja na kuendelea kupanua biashara.

Inabidi uipende shughuli husika unayoifanya, na uweze kutimiza mahitaji ya wateja kupitia biashara husika. Muda wako mwingi utautumia katika shughuli yako mpya utakayojiajiri hivyo, iwapo kazi uliyonayo pengine haikurithishi, hakikisha ajira yako binafsi itakurithisha.

Wafanyakazi ni wa umuhimusana katika kujiajiri.Watendaji wa shughuli husika za biashara yako utakayoianzisha ni muhimu wawe wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha wa kufanya shughuli husika, na uweke mikakati ya kuwapatia nyenzo zote muhimu za kufanyia kazi ikiwemo teknolojia na mazingira mazuri ya kazi. Muda huu ambao umeajiriwa, ndio muda pia muafaka wa kusaka 'vipaji'- yaani watu ambao utafanya nao kazi utakapojiajiri.

Mafanikio yako katika kujiajiri yanategemea mambo mengi ila zaidi sana yanakutegemea wewe. Ni kweli kuwa upo sahihi kufikiria au kuota kufanya biashara kubwa na yenye mafanikio sana, lakini kumbuka mafanikio hayaji kwa usiku mmoja, na hata kama yatakuja kwa usiku mmoja, inahitajika kazi ya muda mrefu kuyafanya yawe endelevu.

## MASWALI

1. Taja aina za ajira.
2. Toa sababu nne zinazoweza kupelekea uajiri wa binafsi.
3. Ndoto ya kujiajiri inafanikishwa na mambo mawili.Yataje.
4. Utafiti kabla ya kujiajiri unahusisha nini kulingana na kifungu?
5. Orodhesha malengo muhimu unayopaswa kushughulikia kabla ya kujiajiri.
6. Taja hoja nne za umuhimu wa kuwa na pesa katika biashara kulingana na kifungu?
7. Ni nini unapaswa kupanga kuhusu pesa kabla ujajiajiri?
8. Toa sababu ya kufahamikiana na wengine kabla ya kujiajiri.

9. Taja vile wakati wa kuajiriwa unakusadai kufahamiana na wengine.
10. Orodhesha njia tatu za kujijenga kimawasiliano na watu kabla ya kujiajiri.
11. Ufahamu wa yanayojiri kila wakati ni muhimu kabla ya kujiajiri. Thibitisha kwa hoja tatu.
12. Ni nini kitasaidia biashara yako kudumu baada ya kujiajiri?
13. Wafanyikazi wako si watu tu wasiolewa.Thibitisha haya kulingana na kifungu.
14. Unawezaje kukidhi mahitaji ya wafanyikazi wako?
15. Fafanua himizo la mwandishi katika aya ya mwisho.

## Mada Ndogo ya 2: Kusoma

### Hali ya ajira na umuhimu wa kujiajiri

Kama ilivyo katika nchi nyingi duniani hasa "zinazoendelea" tatizo la ajira kwa watu wake limekithiri; wasomi, na wasiokuwa wasomi, pia wenye ujuzi na wasiokuwa na ujuzi wote wamekosa ajira.

Kuna sekta mbili za ajira; serikalini na binafsi.Fursa za ajira serikalini zimekuwa ni finyu sana kiasi cha kutokidhi mahitaji ya watafuta ajira. Vijana wengi wamekuwa wakimaliza masomo na mafunzo katika ngazi mbalimbali pasipo kupata kazi za kufanya serikalini. Bajeti finyu inatajwa kuwa kikwazo kikubwa kwa serikali kuajiri au kuweka penyo nyingi za ajira.

Kwa upande wa sekta binafsi, suala la ajira limekuwa likitatuliwa ila sio kwa mafanikio makubwa sana. Sekta binafsi kupitia makampuni, sekta za huduma na ujasiliamari bado hazijaweza kumaliza tatizo la ukosefu wa ajira nchini. Inasemwa kwamba zipo sababu nyingi za ukosefu wa ajiri ikiwa pamoja na; hali duni ya uchumi wa nchi - hivyo sekta binafsi kuajiri watu wachache sana,mifumo migumu ya uanzishaji miradi/biashara binafsi hasa kutoka vyombo vya serikali, ambapo masharti ya kuanzisha biashara mbalimbali yamekuwa magumu na kufanya kuwa kikwazo kikubwa.pia elimu itolewayo mashuleni na vyuoni haiwawezeshi wasomi wanaomaliza kuwa na mawazo ya kutafuta kujiajiri; wengi wao wanawaza kuajiriwa tu .watu wachache wanashikilia uchumi mkubwa wa nchi, hivyo wasio na uwezo kushindwa kufurukuta katika kujiajiri,mifumo kandamizi na migumu ya kibenki ambayo huwakosesha watu wengi sifa za kukopeshwa kwa hivyo maskini wataendelea kukosa fursa za kibenki.

Juu ya hayo wasomi wengi wanadharau kazi mbalimbali aidha kwa kufikiri tofauti au uzembe tu wa kutojua fursa halisi katika mazingira yao. Hatutasahau shida ya watu mwenyewe;uvivu na uzembe wa watu wengi katika utekelezaji wa sera za maendeleo zilizowekwa na serikali. Hapa watu wengi wanaitegemea serikali katika kuweka mazingira yao ya kuajiriwa.

Watu wanatakiwa kujua kuwa japokuwa sekta binafsi ina vikwazo vingi na hasa kujiajiri,sekta hii ni pana kuliko zote, kwa wasomi na wenye ujuzi ifikie mahali waunganishe nguvu zao za kitaaluma na kiujuzi kuanzisha miradi mbalimbali kwa kadri ya fursa za uwekezaji hapa nchini. Mfano vikundivya wasomi wa ngazi fulani kutoka fani mchanganyiko wanauwezo wa kuanzisha kampuni au mradi fulani, huku mifumo ya kibenki ikiwasukuma kwa kutoa mikopo na serikali kuweka mazingira mepesi mwanzoni mwa miradi yao. Kikundi hiki kinaweza kikawa na mradi wa kilimo/kampuni ya kilimo kisha baada ya kuanzisha wakaajiri watu wa kada za kati wenye ujuzi wa kati na wasio kuwa na ujuzi ila wana elimu ya chini.watu wakifanya hivyo, mifumo mingine

inayoonekana imebana itafunguka kwakuwa mifumo hiyo pia inahitaji watu walio na malengo yenye tija.

Kujiajiri kimsingi ni muhimu sana kwa maendeleo ya mtu binafsi na nchi kwa ujumla. Serikali kama imeshindwa kuajiri basi itoe fursa na mazingira mepesi yatakayowafanya angalau wanaotaka kujiajiri watiwe nguvu ya awali.



Vijana wengi  wanaomaliza mafunzo yao, wanataka kuajiriwa ama katika taasisi za serikali, watu binafsi au mashirika ya kimataifa.hata hivyo, si mara zote vijana hawa wanapata kazi mara tu wanapomaliza vyuo.Hii ina maana vijana wanaotamani kuajiriwa serikalini, wanalazimika kusubiri ajira mpya zitakazotangazwa na serikali kwa wakati usiojulikana.katika mazingira kama haya ya kusubiri ajira, vijana wengi huamua kukaa vijiweni, kulala nyumbani, kuzurura mitaani kwa shughuli zisizo na tija, kwa kisingizio cha kusubiri ajira zitangazwe.

Vijana wakingojea ajira wanaweza kujitolea kufanya kazi fulani pasi na malipo au malipo duni tu, kwa maana ya kutumia sehemu ya muda wako, nguvu zako, ujuzi na maarifa uliyonayo kufanya kazi za watu wengine bila kutarajia malipo ya moja kwa moja.kuna sababu kadhaa za kujitolea kwa unayesubiri ajira au wewe unayefanya kazi lakini bado hujaona sababu ya kujitolea;kwanza ni kujifunza ujuzi bila gharama.Si kila ujuzi tunaouhitaji kazini unapatikana vyuoni. Mara nyingi vyuo hutufunza maarifa ya jumla yanayoweza yasioane na

matakwa ya soko la ajira.Ukweli ni kuwa ni vigumu kwa mfumo wa elimu kukidhi mahitaji mahsusi ya kila mhitimu na kila mwajiri. Kwa sababu hiyo, vyuo hujikuta vikifundisha maarifa ya jumla, ambayo katika hali halisi yanaweza yasikidhi mahitaji ya waajiri.Pia, vyuo haviwezi kufanya utafiti wa mara kwa mara kubaini mahitaji halisi ya soko la ajira kwa minajili ya kurekebisha mitalaa yao.katika mazingira haya, kujitolea kunakusaidia kujifunza ujuzi mahususi unaouhitaji ili kuajiriwa kirahisi bila kulazimika kuulipia kwa fedha.

Pili kujitolea kufanya kazi ni njia bora ya kujitafutia uzoefu unaohitajika.waajiri wengi huweka sharti la wanaotafuta kazi kuonyesha uzoefu wa kazi wanayoiomba kama ushahidi wa uwezo wa kumudu kazi husika.Hiki, kwa hakika, ni kikwazo kwa wanaotafuta kazi wengi hasa wanaotoka vyuoni moja kwa moja, kwa sababu ni kweli huwa hawajawahi kuajiriwa na hivyo wanakosa sifa ya uzoefu.Ni vyema tukatambua kuwa waajiri huvutiwa na mwombaji kazi aliye tayari kujitolea. Mwombaji mwenye historia ya kujitolea muda na ujuzi wake kuwanufaisha wengine, anajiwekea nafasi nzuri zaidi ya kuwashinda wenzake wasiojitolea. Kujitolea kunaweza kuwa namna ya kuongeza uwezekano wa kuajirika.

Kuna kila sababu ya kusema kujitolea kufanya kazi bila malipo au malipo duni ni kujiongezea mtandao wa kiajira.Kwa maisha ya sasa, mtandao wa kiajira ni jambo muhimu. Mtu anayefahamiana na watu wengi kwenye maeneo mbalimbali ya kazi, anajiongezea fursa ya kuunganishwa na taarifa nyingi za kiajira.aina ya mitandao ya kiajira tunayoijenga, mara nyingi hutegemea tunafahamiana na watu wa aina gani. Kwa hiyo si kazi nyepesi.Unapokuwa tayari kufanya kazi za kujitolea kwa bidii na maarifa katika maeneo mbalimbali, unakuwa na fursa ya kujitengenezea mtandao muhimu wa watu wanaoweza kukufaa katika safari yako ya kutafuta ajira ya ndoto yako.

Sababu nyingine ni kusaidia kutatua matatizo ya jamii.Maisha ni zaidi ya fedha. Mtazamo huu unaweza kuzua mjadala mrefu kutokana na tofauti za kimtazamo,

lakini upo ukweli kwamba fedha si kila kitu.Hatuishi kwa lengo la kujikusanyia fedha kujiletea faida binafsi na iishie hapo ingawa ni kweli tunahitaji fedha.kujitolea, kwa mantiki hii, ni kuelewa kuwa si lazima ubadilishane ujuzi na muda wako kwa mabulungutu ya fedha. Wakati mwingine unaweza kutoa ujuzi, maarifa na nguvu zako kwa lengo tu la kujisikia furaha ya kutoa mchango wako katika kuboresha maisha ya wengine, ambao katika hali ya kawaida wasingeweza kunufaika na ujuzi huo bila kukulipa.

Ijapokuwa kujitolea kuna faida zake,hata hivyotahadhari unapojitolea.uzoefu unaonyesha kuwa zipo taasisi za kinyonyaji zinazopenda kutumia nguvu za watu bure kwa mwavuli wa kujenga utamaduni wa kujitolea.Taasisi hizi hutumia shida za watu wasio na ajira kujipatia nguvu kazi ya bure bila gharama kubwa ya fedha. Ni vizuri kutambua unyonyaji wa taasisi zenye tabia hii na kufanya uamuzi sahihi utakaokunufaisha na wewe kiujuzi na kiuzoefu.

*Mwandishini mhadhiri wa saikolojia, Chuo Kikuu cha Kikatoliki, Mwenge***.**

## MASWALI

1. Shida ya ukosefu wa kazi inaathiri kina nani kulingana na aya ya kwanza?
2. Taja aina mbili za sekta ya kuajiri watu.
3. Ni vipi serikali inasababisha ukosefu wa ajira?
4. Ni sekta zipi ambazo zimejaribu kutatua shida ya ukosefu wa ajira?
5. Orodhesha sababu kumi za ukosefu wa ajiri.
6. Ni yepi matokeo ya watu wachache kumiliki uchumi wanchi?
7. Sekta ya benki inawakandamiza watu kwa njia zipi?
8. Wasomi wanaweza wakachangia tatizo la ukosefu wa ajira vipi?
9. Thibitisha matukio matatu yanayoonyesha kutowajibika kwa vijana wakingojea kuajiriwa.
10. Eleza dhana ya ‘kujitolea’kufanya kazi.

11. Kujitolea kunasaidia vipi kwa kutotumia pesa zako?
12. Eleza manufaa ya uzoefu wa kazi kabla ya kuajiriwa.
13. Eleza maana ya''kujitolea kufanya kazi bila malipo au malipo duni ni kujiongezea mtandao wa kiajira.''
14. "Kujitolea, kwa mantiki hii, ni kuelewa kuwa si lazima ubadilishane ujuzi na muda wako kwa mabulungutu ya fedha." Thibitisha haya kwa hoja za mwandishi za kujitolea bila malipo.
15. Mwandishi anatoa tahadhari ya kujitolea kwa nini?

## WASIFUKAZI

Wasifu wa kazi ni taarifaya inayosimulia maisha ya mtu, tangu kuzaliwa kwake, elimu, ujuzi wa kazi na uzoefu. Umuhimu wa nyaraka hii siyo tu kwa watafuta ajira lakini hata wale wenye ajira tayari. Wasifu wa kazi husaidia kuonyesha uwezo na ubora wako wa kitaaluma na katika utendaji wa kazi.

Wasifu pia ni nyaraka inayoweza kukusaidia kuuza ujuzi wako kwa watu na mashirika ambayo yanaweza kuhitaji kukuajiri au kukutumia katika shughuli fulani.

Umuhimu wa wasifu wa kazi unaonyesha dhahiri kuwa ni kitu kinachotakiwa kiandaliwe kwa ustadi na umakini mkubwa. Pamoja na ukweli huu bado kuna makosa ya mara kwa mara ambayo yamekuwa yakifanywa na waandishi wengi wa wasifu. Makosa haya yanayofanya nyaraka hii muhimu ya wasifu kazi kukosa ushawishi na pengine kupuuzwa na waajira hasa kwa wale wanaotafuta ajira.Je ni makosa yapi yanaweza kufanya wasifu wako usionekane bora?

Kwanza ni makosa ya kiuandishi. Kutokana na kukosa umakini au kutojiridhisha baada ya kuandaa wasifu, makosa mengi ya kiuandishi huonekana kwenye nyaraka hii. Unapoandaa wasifu wako ni vyema kupitia mara kadhaa na kujiridhisha kama hakuna makosa yoyote ya kiuandishi. Unashauriwa pia kumpa mtu mwingine akusaidie kupitia kama kuna makosa mengine yoyote unayoweza

kuwa umeyaacha. Ifahamike kuwa waajiri wanaweza kuachana kukuita kwenye usaili kwa sababu tu wasifu wako una makosa ya kiuandishi.

Pili ni uandishi usiowiana katika wasifu kazi.Wasifu wako unatakiwa kuwa na mtindo na ukubwa wa maandishi unaowiana.Wasifu unapochapwa kwa kompyuta unaweza kuandika kwa kutumia mitindo mbali mbali ya maandishi.Hakikisha unatumia mtindo mmoja kwa wasifu wote huku ukubwa wa maandishi pia ukiwa sawa japo unaweza tofautisha kwa kuonyesha tofauti ya maandishi katika vipengele au vichwa. Ikumbukwe kuwa vichwa vyote vinatakiwa kuwa sawa pia. Hakikisha hutumii rangi nyingi katika wasifu wako. Rangi nyeusi pekee inafaa kwa kuandika wasifu wako wote.

Epuka yasiyokuwa muhimu katika wasifu kazi.Siyo kila kitu ni cha kuandika au kuweka kwenye wasifu wako wa kazi.Unapotaka kuweka au kuongeza kitu kwenye wasifu wako wa kazi jiulize kama kina uhusiano na hiyo kazi au kinaweza kukuuza vipi kwa mwajiri.Baadhi ya mambo yanapoandikwa au kuwekwa kwenye wasifu yanaweza sababisha ukabaguliwa au kuonekana haufai kwa kazi husika. Mambo kama imani yako ya dini si muhimu kwani hayana msaada wowote kwenye kushawishi kuajiriwa kwako na yanaweza sababisha ukabaguliwa kama anayepitia wasifu atakuwa wa imani tofauti au inayokinzana na yako.Kama unaomba ajira kwenye shirika la dini na unahisi kutaja dini yako kutakuongezea nafasi ya kuchaguliwa au kuajiriwa si vibaya kuainisha imani yako.

Endapo unaomba ajira na mwajiri hajaainisha kuwa uweke picha yako pia si vyema kuambatanisha kwenye wasifu wako kwani inaweza kuwa chanzo cha kubaguliwa kwa sababu mbalimbali.Je, unahisi wewe una sura nzuri sana hivyo itashawishi kuajiriwa kwako? Kama jibu ni ndiyo, inaweza isikusaidie na ikakuletea madhara. Yupo mtu anaweza akajisemea tu, “Huyu alivyo mzuri tukimchagua atakuja kuongeza ushindani na kutunyakulia mabwana zetu hapa”.

## Mfano wa wasifukazi

**Wasifu**

| | |
|---|---|
| Vijalizo vya Jina | Mhe. |
| Jina la Ukoo: | Majaliwa |
| Jina la Kwanza: | Kassim |
| Jina la Kati: | Majaliwa |
| Tarehe ya Kuzaliwa: | 1960-12-22 |
| Mahali Alipozaliwa: | |
| Hali ya Ndoa: | Nimeoa |
| Kundi: | Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano |
| Jinsia: | M |
| Simu ya Ofisi: | - |
| Simu ya mkononi: | 785205910 |
| Barua pepe: | majaliwa.kasimu@yahoo.com |
| Anuani: | P.O.Box 51,<br>Ruangwa |

**Elimu**

| Toka | Hadi | Jina la Shule/Chuo | Cheti |
|---|---|---|---|
| 1970 | 1976 | Mnacho Primary School | cheti cha Elimu ya Msingi |
| 1977 | 1980 | Kigonsera Secondary School | CSEE |
| 1991 | 1993 | Mtwara Teachers College | - |
| 1994 | 1998 | University of Dar es Salaam | Bachelor Degree |
| 1999 | 1999 | Storckolm University | PGDP |

**Mafunzo Mengineyo**

-

**Uzoefu**

| Toka | Hadi | Jina la Mwajiri | Ngazi/Wazifa |
|---|---|---|---|
| 2010 | 2014 | - | MB |
| 2006 | 2010 | PM | Mkuu wa Wilaya |
| 2001 | 2006 | PS-CWJ | Katibu Mkoa |
| 2001 | 2001 | PS-CWJ | Katibu Wilaya |
| 1988 | 2000 | PS-Moec | Mkufunzi |
| 1984 | 1986 | TD-Lindi Council | Mwalimu |

**Burudani**

- Kadanda

Michango Maswali Maswali ya Nyongeza

Wasifu kazi huandamana na mahitaji. Kila kazi ina mahitaji yake, hata kama umeuandika wasifu wako kwa ustadi wa hali ya juu kumbuka kwamba hauwezi kutumia huo wasifu kwa matumizi yote. Kama unaomba kazi ya uhasibu, wasifu utakaoutumia hautakiwi kuwa sawa na ule utakaoutumia ukiwa unaomba kazi ya ofisa wa benki. Kila kazi ina mahitaji yake, hivyo unatakiwa uhakikishe kuwa wasifu wako unakidhi mahitaji ya kazi husika.Ujuzi wa kazi moja mara nyingi siyo ujuzi wa kazi nyingine hivyo ni muhimu kuzingatia mahitaji ya kazi husika.

Urefu wa wasifu wa wasifu ni jambo la kuzingatia.Watu wengi hudhani kuwa, kuwa na wasifu wenye kurasa nyingi kuna kupa nafasi ya kuonekana wewe ni bora kuliko yule mwenye wasifu wenye kurasa chache lakini kinyume chake kinaweza kuwa sawa kwa baadhi ya mazingira. Waweza andaa wasifu wa kurasa kumi lakini mwenye wasifu wenye kurasa mbili tu akaonekana ni bora zaidi kuliko wewe.Ni vyema kuzingatia vitu vya msingi vya kuweka kwenye wasifu wako na kuviweka katika mpangilio mzuri. Haina haja ya kuonyesha alama ulizopata kwa kila somo ulipokuwa chuoni. Kama mwajiri atahitaji hili ambatanisha matokeo yako. Lakini ikumbukwe pia kuwa baadhi ya kazi kamauhadhiri wasifu utahitaji kuonyesha idadi ya machapisho ya kitaaluma aliyoyachapisha muhusika bila kujali idadi hivyo ni urefu wa wasifu katika mazingira haya unaweza usiwe shida.

Ni makosa kutoa taarifa zisizo sahihi ili kuwashawishi waajiri. Wapo watu wanaoamua kutoa taarifa zisizo za kweli kwa lengo la kuwahadaa waajiri. Moja ya vipengele vinavyoongoza katika kuweka taarifa zisizo za kweli ni kile cha uzoefu.Kwa namna teknolojia ilivyokua, ni rahisi kwa mtu kujiridhisha kama ni kweli taarifa ulizozitoa ni za kweli au ni vinginevyo. Kusema kwamba ulishawahi kufanya kazi na shirika fulani wakati siyo kweli kunaweza kukufanya uonekane si mwaminifu na hivyo kuharibu sifa yako.Wadhamini uliowaweka wanaweza kupigiwa simu kujiridhisha pia hata hilo shirika ulililoliainisha kwenye wasifu wako laweza kupigiwa simu.

## MASWALI

1. Taja wale wanapaswa kuandika wasifu kazi.
2. Fafanua umuhimu wa wasifu kazi.
3. Taja athari ya tawasifu yenye makosa.
4. Makosa ya kimaandishi katika tawasifu yanaweza kutokea kwa sababu ya mambo mawili.Yataje.
5. Eleza njia mbili za kuhakikisha wasifu kazi wako hauna makosa ya kimaandishi.
6. Fafanua maana ya uandishi usiowiana wa tawasifu.
7. Vichwa katika wasifu kazi vinaandikwaje?
8. Ni rangi ipi inapendekezwa kwa maandishi ya wasifu kazi?
9. Taja vitu viwili vinavyoweza kumkosesha kazi mtu akiviweka katika wasifu kazi ikiwa haujaombwa kufanya hivyo.
10. Wakati mwafaka wa kutaja dini yako katika wasifu kazi ni upi?
11. Ujuzi wa kazi moja mara nyingi siyo ujuzi wa kazi nyingine hivyo, ni nini ambacho ni muhimu kuchunguza hapa unapoandika wasifu kazi?
12. Ni yepi ya kuzingatia katikaurefu wa wasifu kazi?
13. Taja kile unaweza kuacha nje ili kupunguza urefu wa wasifu kazi.
14. Ni sehemu ipi ambayo watu wengi wanadanganya katika wasifu kazi?
15. Eleza madhara ya kutosema ukweli katika wasifu kazi.

**Mada Ndogo ya 3:** **SARUFI**

## Viambishi

Kiambishi ni silabi inayofungamanishwa na mzizi wa neno ili kuleta maana iliyokusudiwa. Viambishi havina maana kamilifu peke yake: huhitaji kufungamanishwa na mzizi wa neno. Kwa hivyo, kiambishi ni mofimu tegemezi inayoongeza maana fulani katika neno kama vile ngeli, wakati, hali, mnyambuliko wa kitendo n.k.

Kuna aina mbili kuu za viambishi:

1. Viambishi awali
2. Viambishi tamati

## Viambishi Awali

Viambishi hivi huongezwa au kuambishwa kabla ya mzizi wa kitenzi. Huwa na majukumu mbalimbali:

1. *Viwakilishi nafsi:* Huonyesha nafsi inayozungumziwa kama iko katika umoja au wingi.
2. *Viambishi awali vya wakati/hali:* Huonyesha wakati au hali ya kitendo.
3. *Vikanushi:* Huashiria kukanusha kwa kitenzi.
4. *Virejeshi:* Hivi ni viambishi vinavyomrejelea mtenda wa jambo.
5. *Viambishi vya mtendwa au mtendewa:* Huonyesha anayetendewa jambo au anayetendwa.
6. *Vipatanishi vya ngeli:* Huonyesha upatanisho wa ngeli. Hivi hutegemea ngeli inayohusika.

## Viambishi Tamati

Hivi viambishi ni vile vinavyoambishwa baada ya mzizi wa kitensi. Viambishi hivi huwa na majukumu tofauti tofauti.

1. *Kiishio:* Kiambishi hiki huonyesha mwisho wa kitenzi. Kwa kawaida, vitenzi vya Kiswahili huishia kwa kiambishi 'a' katika hali ya kwawaida kwa vitenzi vya Kibantu. Vyenye asili ya kigeni huweza kuishia 'u' au 'i'.
2. *Virejeshi:* Hivi ni viambishi ambavyo hurejesha kwenye mtenda au mtendewa.
3. *Viambishi vya mnyambuliko:* Huonyesha kauli mabalimbali za kitenzi au vitenzi vinavyohusika.
4. *Viambishi vya kuonyesha rai au amri:* Viambishi vinavyotumiwa kuonyesha rai, au pendekezo ni e, (katika umoja) na –eni (katika wingi).
5. *Viambishi vya mahali:* Katika baadhi ya vitenzi viambishi vya mahali –po, -ko, -mo humabishwa mwishoni mwa vitenzi kuashiria mahali.

### Zoezi

**Onyesha viambishi mbalimbali katika maneno yafuatayo.**

1. yanayotumiwa
2. unachoona
3. imesimuliwa
4. ulimwangukia
5. alifanyishwa
6. atakapovuna
7. umenunuliwa
8. huchelewa
9. nimekuuliza
10. nendeni

## Mada Ndogo ya 4: Kuandika

1. Andika wasifu kazi wa kutafuta kazi.
2. Uaminifu katika kazi ni muhimu. Jadili.
3. Mtu si lazima aajriwe anaweza kujiari. Eleza changamoto za kujiajiri.

## Mada Ndogo ya 5: Msamiati

**Tarakimu**

Tarakimu ni kuendeleza alama ya hesabu ili kuonyesha idadi.

Mifano;

0 - sufuri
10 - kumi
100 - mia moja
1,000 - elfu moja
10,000 - elfu kumi
100,000 - elfu mia / laki moja
1,000,000 - milioni moja
10,000,000 - milioni kumi
10,000,010 - milioni kumi na kumi
10,000,050 - milioni kumi na hamsini

20,000,000 - milioni ishirini

30,000,000 - milioni thelathini

40,000,000 - milioni arobaini

50,000,000 - milioni hamsini

60,000,000 - milioni sitini

70,000,000 - milioni sabini

80,000,000 - milioni themanini

90,000,000 - milioni tisini

100,000,000 - millioni mia moja

1. Shamba hilo lilinunuliwa shillingi 99,000,000.
   Shamba hilo lilinunuliwa shillingi milioni tisini na tisa.
2. Benki kuu ilikopesha shillingi 1,200,000.
   Benki kuu ilikopesha shillingi milioni moja, laki mbili.
3. Wanamazingira wamepanda miti 17,735,350 kwa miaka kumi.

Wanamazingira wamepanda miti milioni kumi na saba, laki saba thelathini na tano elfu, mia tatu na hamsini.

## Zoezi

a) Andika tarakimu zifuatazo kwa maneno.

1. 111,001
2. 342,002,020
3. 696,696
4. 277,001,340
5. 500,505,005
6. 126,262
7. 777,070,070
8. 100,000,010
9. 952,333,303

10. 10,001,001

**b) Andika tarakimu zifuatazo**.

1. Elfu mia moja na kumi na moja.
2. Laki sita na sita.
3. Kumi na tano elfu.
4. Laki moja, tisini na tisa elfu na tano.
5. Robo milioni.
6. Milioni saba, laki saba kumi na saba.
7. Milioni nne unusu.
8. Sabini na tatu elfu.
9. Milioni mbili na mbili.
10. Laki tatu na thelathini na tatu.

## Akisami

Akisami ni sehemu ya kitu. Mifano;

1. - nusu
2. - thuluthi
3. - robo
4. - humusi
5. - sudusi
6. - subui
7. - thumni
8. - tusui
9. - ushuri
10. - thuluthi mbili

12. - subui tano
13. - tusui sita
14. - thuluthi mbili
15. - humusi nne
16. - ushuru mbili
17. - subui nne
18. - tusui tatu
19. - thumni sita
20. - sita kwa kumi na sita
11. - robo tatu

## Zoezi

**A. Tunga sentensi ukitumia maneno haya.**

1. maridhawa
2. mwafaka
3. saba
4. bora
5. laini
6. nadhifu
7. shwari
8. dhaifu

**B. Kosoa sentensi zifuatazo.**

1. Msichana mhodari alipewa vitabu visaba.
2. Kiti kiduni kilivunjika kwa sababu kilikuwa kidhoofu.
3. Maswali masita yalikuwa marahisi sana.
4. Vitafunio virojorojo na vilaini vililetwa na wageni.
5. Alipanga manguo malaini kwenye kabati.